Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Arobaini na Moja - Tarehe 5 Agosti, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Taarifa ya Mwaka ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa Mwaka 2002/2003 *(The Annual Report of the Institute of Finance Management for the Year 2002/2003).*

Hati za Uhamishaji Fedha Na. 1,3 na Na. 4 za Mwaka 2003/2004 *(Statement of Reallocation Warrant No. 1, 3 and No.4 of 2003/2004).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 385

**Barabara za Katoro - Nyarugusu na Katoro - Kanema**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa mawasiliano kwa njia ya barabara ni muhimu kwa wananchi katika kujikwamua na umaskini na kwa kuwa barabara ya Katoro - Rwangasa - Nyarugusu na ile ya Rwangasa- Ibondo - Shilabela - Msasa - Busanda - Genge Saba - Kasungamile - Nyabulolo hadi Kamena hazijafanyiwa ukarabati kwa zaidi ya miaka 30 hadi leo.

(a) Je, kwa muda wote huo ni kweli kwamba Serikali haijawahi kupata fedha?

(b) Je, Serikali haioni kwamba imedhamiria kuwatesa wananchi wa maeneo hayo?

(c) Je, Serikali inawaahidi nini wananchi hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya Katoro - Ibondo - Silabela - Msasa - Busanda - Genge Saba - Kasungamile - Nyabulolo hadi Kamena ina umbali wa kilometa 54 ambayo ni ya udongo, inaziunganisha tarafa za Busanda na Nyang'hwale. Barabara hii ni ya vijijini *(feeder road).* Aidha, barabara ya Katoro- Rwamgasa - Nyarugusu ina urefu wa kilometa 48 na ni ya udongo. Barabara hii ilikuwa ya kijiji iliyotengenezwa kwa nguvu za wananchi. Barabara hii ilipandishwa daraja mwaka 1998 na kuwa ya Wilaya ambapo inatakiwa kuhudumiwa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2000/2001, Serikali kupitia Mfuko wa Barabara, ilifanya matengenezo katika barabara ya Katoro- Kanema katika sehemu ya Genge Saba - Kasungamile - Nyabulolo kwa kujenga vivuko *(culverts)* kwa gharama ya jumla ya shilingi 6,588,382.00. Nia kubwa ilikuwa kupunguza sehemu korofi za vivuko ili ziweze kupitika hata wakati wa masika. Katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali kupitia mfuko wa barabara iliendelea kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Katoro - Rwamgasa - Nyarugusu sehemu ya Katoro - Rwamgasa yenye urefu wa kilometa 18 kwa gharama ya shilingi 9,344,960/=.

(b) Mheshimiwa Spika, si dhamira ya Serikali kuwatesa wananchi wake, bali ni nia ya Serikali kuboresha mawasiliano ya barabara nchi nzima. Tatizo ni ufinyu wa bajeti unaofanya uboreshaji wa miundombinu kufanyika kwa awamu. Barabara hizi zinahitaji matengenezo makubwa na kwa kuona umuhimu huu Serikali kwa mwaka wa fedha 2004/2005 imepanga kufanya matengenezo ya sehemu korofi umbali wa kilometa 16 kwenye barabara ya Katoro - Kamena sehemu ya Ibondo - Shilabela - Msasa katika awamu ya kwanza na awamu ya pili itahusisha barabara ya Katoro - Rwamgasa.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Waziri amekiri kabisa kwamba barabara hii ina kilometa 54 na matengenezo yake kwa awamu zote hizo wametoa shilingi milioni 15 tu. Je, haioni kwamba barabara hii hawatendei haki na wananchi wa kule hawatendewi haki?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu la Mheshimiwa Ernest Mabina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika kipindi hicho zimetumika shilingi milioni 15 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii. Lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hii inatokana na ufinyu wa bajeti. Vile vile napenda kusisitiza kwamba nchi yetu ni kubwa na barabara za vijijini zina urefu mkubwa sana, ufinyu wa bajeti ndiyo unaosababisha tusiweze kuzishughulikia barabara zote kwa wakati mmoja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara za Wilaya ya Geita na Wilaya zingine zinazohudumiwa na Halmashauri za Wilaya, ikiwemo ile ya kutoka Nyang'hwale kwenda Mungiro hadi Nyamikonze na ile ya Buharahara kupitia Shabaka hadi Nyang'hwale ni mbaya sana na kwa kuwa bajeti za Halmashauri haziwezi kukidhi mahitaji ya barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mpango gani wa kijumla wa kutengeneza barabara za vijijini ukizingatia kwamba uchumi wa nchi sasa ni mzuri na tunasamehewa hela nyingi zinarudi kwa mpango wa *HIPC? (Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tatizo ni ufinyu wa bajeti. Serikali huwa inatoa fedha kutokana na mfuko wa barabara ndiyo zinagawiwa kidogo kidogo. Hii inahusu Halmashauri zote na siyo Halmashauri ya Wilaya ya Geita peke yake. Naamini kwamba jinsi tunavyozidi kuendelea fedha zitakuwa zinapatikana, kwa uchache huo huo na tutakuwa tunaendelea na matengenezo.

Na. 386

**Semina na Mafunzo Mbalimbali kwa Madiwani Wanawake**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa nia mojawapo ya kuwa na Madiwani Wanawake ni kuwawezesha kuwa na wawakilishi wa wananchi husika katika vyombo vya maamuzi kama vile Halmashauri na kwa kuwa ili kiongozi aweze kutekeleza wajibu wake kwa uhakika na kwa kitalaam ni lazima awe anafahamu wajibu/majukumu yake ambayo anakuwa amefahamishwa kwa njia mbalimbali kama vile semina, vijitabu na vipeperushi vinavyoelezea majukumu hayo, kujifunza kwa kutembelea Halmashauri nyingine ndani na nje ya nchi kama wanavyofanyiwa Wabunge wengine ili kuona utekelezaji wa majukumu mbalimbali mfano Madiwani kutosimamia utoaji wa asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya wanawake na vijana.

(a) Je, ni Halmashauri ngapi zimetoa semina au kutembelea Halmashauri nyingine kwa Wanawake wa Viti Maalum?

(b) Je, ni Halmashauri zipi ambazo bado hazijatoa mafunzo hayo na zitatoa mafunzo ya aina hiyo lini?

(c) Kwa Halmashauri ambazo hazijatoa mafunzo hayo kwa walengwa, hazioni kwamba zinasababisha kuwa na wanawake wawakilishi ambao hawajui vyema wajibu na majukumu yao na hivyo kuwafanya washindwe kuchangia maendeleo ya wanawake na badala yake kuishia kupata posho tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika utaratibu unaoendelea wa maboresho ya Serikali za Mitaa, kila Halmashauri inayo Kamati ya maboresho ambapo upo mpango maalum wa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri na pia Madiwani wote bila kubagua wanawake au wanaume. Mafunzo hayo yanasaidia kufahamu mabadiliko yanayojitokeza kulingana na maboresho. Mafunzo yanayotolewa yanahusu masuala ya menejimenti, fedha, uwajibikaji na utendaji kwa ujumla. Kwa kupitia vitengo vya maboresho vya kanda, mafunzo haya yametolewa katika Halmashauri zote kwa nyakati mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa misingi ya maelezo yangu katika jibu (a) hakuna Halmashauri ambayo haijapatiwa mafunzo niliyoyaelezea aidha, ofisi yangu pia inayo programu ya mafunzo kwa Madiwani wote waliopo nchini. Mafunzo yalifanyika kuanzia mwezi Machi, 2003 kwa miezi minane mfululizo na yalitolewa kwa Madiwani wote 2,537 wanawake na wanaume. Mafunzo haya yalihusu sheria na mabadiliko katika mfumo wa Serikali za Mitaa, wajibu na majukumu ya Diwani katika uongozi na uendeshaji wa Serikali za Mitaa, utoaji wa huduma na uhamasishaji wa maendeleo katika Serikali za Mitaa na usimamizi na udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Halmashauri isiyoendesha mafunzo kwa watumishi na Madiwani wake wakiwemo Madiwani Wanawake, itawafanya wasifahamu vyema wajibu na majukumu yao na hivyo kushindwa kuchangia maendeleo. Kwa kuelewa umuhimu huu ndiyo maana Serikali na Halmashauri zinazo programu kabambe za mafunzo kupitia mpango wa maboresho ili kuwawezesha watumishi na Waheshimiwa Madiwani wote kufahamu majukumu yao ipasavyo.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutoa mafunzo haya. Nina swali moja tu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge, kwa utaratibu wa sheria ya Halmashauri ni Madiwani. Je, inakuwaje Wabunge hawa hawapati semina hizo kama wanavyopata Madiwani wengine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Waheshimiwa Wabunge, kwa nyadhifa zao ni madiwani vile vile. Lakini suala la kupanga ni lini mafunzo haya yanaendeshwa inategemea vile vile utaratibu wa Halmashauri. Tutawahimiza Wakurugenzi kuhakikisha kwamba wanawaarifu Waheshimiwa Wabunge, wakati mafunzo hayo yanapoendeshwa ili waweze kuhudhuria. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Waziri, ameonyesha kwamba mafunzo haya ni muhimu na yanaweza kusaidia sana uendeshaji wa Halmashauri. Je, Serikali haioni ni bora mafunzo haya yakafanyika mara baada ya uchaguzi kuliko kusubiri muda mrefu baada ya miaka miwili ambapo muda wa Madiwani karibia unaisha ili kuweza kuboresha Halmashauri zetu vizuri? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunawajibika kuendesha mafunzo haya mara baada ya uchaguzi kama ambavyo tunakusudia kufanya mwaka 2006. Lakini mafunzo haya yana gharama kubwa na kwa bahati mbaya mafunzo haya yanaendeshwa kwa fedha za wafadhili. Sasa inategemea upatikanaji wa fedha hizo. Katika kipindi kilichopita wafadhili walichelewa kutoa fedha hizo.

Na. 387

**Wizi wa Vifuniko vya Mashimo ya Majitaka**

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE (k.n.y. MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF)** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa biashara ya *scrap metal* imeshamiri sana hapa nchini na kwa kuwa wanunuzi wanaopelekewa malighafi hiyo nje ya nchi hawajali kuwauliza wanaowapelekea mali hiyo, kwamba wanaipata wapi na kwa kuwa Serikali imeacha kila kitu kiamuliwe na soko huria bila kujali madhara yanayoweza kutokea kwa nchi na kwa kuwa kumetokea mtindo wa watu kuiba mifuniko ya chuma cha pua inayoziba mashimo ya mifereji ya maji taka na kuiuza kama *scrap* na kuyaacha mashimo hayo yakiwa wazi

kwenye maeneo ya miji yetu hapa nchini na hasa Dodoma na kusababisha watu na magari kutumbukia na kusababisha ajali mbaya.

(a) Je, kwa nini Serikali imelifumbia macho tatizo hilo na itaendelea kulifumbia macho mpaka lini?

(b) Kwa kuwa Serikali inalifahamu tatizo hilo, je, sasa ina mikakati gani ya kukomesha wizi huo mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO NA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chuma cha *cast iron* ambacho hutengeneza mifuniko ya chemba za mifumo ya majitaka ni mojawapo ya aina ya vyuma vinavyokatazwa kuuzwa nje ya nchi, kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 170 la mwaka 2003), vyuma vingine ni *medium tensile steel, stainless steel, aluminium* na *brass.* Mantiki ya tangazo hili ni kuwapa nafasi wafanyabiashara na wenye viwanda wa hapa nchini kuimarisha shughuli zao.

Kwa vile biashara hii sasa imebakia ni ya ndani ya nchi tu, ni rahisi zaidi kuratibu na kudhibiti wafanyabiashara na wenye viwanda wachache wasiokuwa waaminifu. Hivyo Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi nyingine inaangalia hatua zaidi zinazostahili kuchukuliwa kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtandao wa majitaka wa Manispaa ya Dodoma ni kwamba ulikabidhiwa na *CDA* kwenda kwenye Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dodoma *(DUWASA)* mwezi Februari, 2002 ukiwa na jumla ya chemba 709. Kati ya hizo mifuniko ya chembe 70 ilikuwa imekwishaibiwa. Aidha, mifuniko 48 zaidi yenye thamani ya shilingi 7,600,000/= iliibiwa kuanzia wakati huo hadi mwezi Machi, 2004 na kufanya jumla ya mifuniko iliyoibiwa kufikia 118. Kutokana na hali hii, Wizara yangu kupitia *DUWASA* imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuyatambua makampuni yanayojishughulisha na ununuzi wa vyuma chakavu katika Mji wa Dodoma ambapo makampuni saba yameshatambuliwa na taarifa kufikishwa katika vyombo vya dola Mkoani Dodoma ambapo utawala Mkoani Dodoma umeshapiga marufuku tayari kuhusisha biashara hiyo ya vyuma chakavu.

(ii) Kuimarisha mifuniko ya chemba iliyobaki kwa njia ya kuchomelea *spot welding.*

(iii) Kufanya ukaguzi mara kwa mara katika mtandao ili kudhibiti uhalifu huo.

(iv) Kutoa matangazo kwa wakazi wa Mji wa Dodoma kupitia katika vyombo vya habari ili waweze kutoa taarifa pindi wanapobaini kuwepo matukio kama hayo.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zimeanza kuonyesha mafanikio kwani tangu zilipoanza kuchukuliwa takribani miezi miwili iliyopita, hakuna mifuniko iliyoibiwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba wananchi wa Dodoma na Miji mingine kushirikiana kwa karibu na uongozi wa Dodoma na Manispaa ya Dodoma ili kuhakikisha kwamba wanadhibiti uhalifu huo na wanalinda vifaa vya miundombinu ya majisafi na majitaka ili shughuli hiyo ifanyike kwa ufanisi. Pale ambapo wahalifu wanakamatwa, wafikishwe kwenye vyombo vya sheria ili waweze kuadhibiwa.

**MHE. DR. HASSY H. B. KITINE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna makampuni saba yaliyobainishwa kama yanaweza kusaidia kushughulikia tatizo hilo ambalo limeulizwa katika swali. Je, hayo makampuni ni yapi na majina yake ni yapi? Ningependa kufahamu kwa niaba ya Mheshimiwa Saggaf.  Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr.Hassy Kitine, kama ifuatavyo:-

Kwanza makampuni niliyoyataja yanajishughulisha kama *agents* wa kukusanya vyuma chakavu. Makampuni tuliyobaini mengi yake *based ni Dar es Salaam* na hapa yanafanya kazi kama *branches.* Sasa kwa vile swali la msingi halikutamka kwamba tutoe majina ya makampuni ambayo yanafanya hiyo biashara, namwomba Mheshimiwa Mbunge kama atahitaji orodha hiyo tuweze kui-*extract* kutoka kwa Msajili wa Makampuni ili tumpatie. Lakini hivi hivi tu itakuwa ni vigumu sana bila kufuata utaratibu.

Pili, ningependa nimweleweshe kwamba uzoefu umetuonyesha kwamba hawa wanaonunua *scrap* mara nyingi *scrap* hiyo inakataliwa inapofikishwa kwenye viwanda vya kuyeyusha chuma kwa mfano kama *cast iron, cast iron* siyo nzuri kwa kutengeneza nondo ambazo ndiyo zinatumika sana na viwanda hivi vya hapa.

Kwa hiyo, *scrap* ambazo huwa wanahitaji *actually* ni *(milled steel)* ambayo ikiyeyushwa wanatengeneza nondo baada ya kupata *high tensile* au *medium tensile steel.*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa kupata nafasi kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa madhara ya kuibiwa mifuniko hii si kwa Mji wa Dodoma tu lakini hata Dar es Salaam na ni kipindi kirefu mashimo haya yameachwa wazi kwa hiyo, kuleta ajali za magari pia vile vile hata wasafiri wa miguu kuanguka katika mashimo hayo, je, Serikali inatamka nini katika kurekebisha hali hii kwa haraka ili Taifa na wananchi wasipate usumbufu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shekiffu kama ifuatavyo:-

Serikali kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba imepiga marufuku upelekaji nje wa chuma chakavu na tunaendelea kusema hivyo tena kwamba tangazo lile tulilotoa la kupiga marufuku linaendelea kushamiri na kuendelea kutekelezwa. Kwa hiyo, mtu yeyote kwa kwali anayepeleka chuma nje anavunja sheria. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu suala hilo kama ifuatavyo:-

Kwanza kwa Mji wa Dodoma kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, suala hili limepigwa marufuku na waliopiga marufuku ni Manispaa ya Dodoma. Tuwaomba vile vile viongozi wengine hao wanaozungumzwa wa Dar es Salaam wachukue hatua zinapaswa kama wenzao wa Dodoma walivyofanya. *(Makofi)*

**MHE. HASHIM A. Z. SAGGAF:** Mheshimiwa Spika, utanisamehe sana. Pamoja na majibu mazuri nimesoma hapa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa niulize swali moja tu kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa hii mafuniko ambayo inaibiwa pamoja na mabomba ya madaraja na kadhalika mwishoni huwa yanaishia kwenye ile tunaita *informal sector. Informal sector* inafanya kazi kwa madhara ya *formal sector.*

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni ya kuwa kwa kuidekeza *informal sector* namna ilivyo ya kuwa hii Serikali inatumia kiini macho kwa kutowawekea utaratibu na masharti maalum ya kufanya biashara zao? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hashim Saggaf, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo kama ifuatavyo:-

Kwanza suala la hawa wanaochukua chuma ni kweli sehemu inakwenda kwenye *informal sector* na tunaandaa utaratibu mpya wa leseni za biashara ambao hawa wote watakaokuwa wanafanyabiashara katika *informal sector* na wenyewe pia wataandikishwa kwa hiyo, watajulikana na hivyo kuondoa tatizo la hawa wafanyabiashara ambao hawatakuwa wanajulikana. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, wale wote ambao wanaoiba mifuniko ya mifereji ya maji machafu au maji safi hao ndiyo maana tumepiga marufuku hiki chuma. Hiki chuma cha *cast iron* wanaotumia ni watu wawili tu ambao ni *Tanzania Railways Corporation* na Nyumbu basi na wao wanajua hilo, wengine wote chuma cha *cast iron* hawakitumii. Kwa hiyo, ndiyo maana soko lake ni *limited* na hawa wanajua hawawezi kuchukua mifuniko. Ahsante.

Na. 388

**Maji Safi na Salama kwa Matumizi ya Binadamu**

**MHE. PAUL E. NTWINA** aliuliza:-

Kwa kuwa hakuna majisafi na salama kwa matumizi ya binadamu katika maeneo ya Kapalala, Kininga, Patemela, Miembeni, Iseche, Mbala, Namkukwe Isanzu, Mheza, Malangali, Mpona, Iyovyo, Itindi, Ndalyongo, Ileya na Totowe na kwa kuwa Serikali imevipatia maji ya visima vijiji vichache vya Galula, Mbuyuni na Mbagala ingawa pampu hazijafungwa na kwa kuwa vijiji hivyo vinategemea sana maji ya Mto Songwe na ziwa Rukwa ambayo ni machafu sana.

(a) Je, ni lini vijiji hivyo vitapatiwa maji safi kwa matumizi ya kila siku ya binadamu?

(b) Je, kwa nini kusiwe na mikakati madhubuti ya kutatua matatizo ya maji nchini hususan katika Jimbo la Songwe?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ntwina, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa vijiji vya Kapalala, Kininga, Patamela, Miembeni, Iseche, Mbala, Namkukwe Isanzu, Mheza, Malangali, Mpona, Iyovyo, Itindi, Ndalyongo na Totowe havina maji safi na salama kwa matumizi ya binadamu. Kijiji cha Ileya kinapata maji safi na salama kutoka katika mradi wa maji wa Ifwenkenya uliofadhiliwa na Serikali ya Denmark. Vijiji vya Kapalala na Kininga vilikuwa na huduma ya maji kutokana na mradi uliojengwa mwaka 1984 katika maeneo hayo. Hata hivyo, mashine ya maji iliibiwa katika mradi huo na hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, ili kuwapunguzia wananchi wa Jimbo la Songwe, tatizo la maji, Serikali imetenga shilingi milioni 20 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kununua na kufunga pampu nne za mkono na pampu moja ya dizeli kwenye visima vitano vilivyochimbwa mwaka 2003 katika Vijiji vya Galula, Mbuyuni na Mbagala katika Jimbo la Songwe.

Pamoja na jitihada hizo za Serikali, namwomba Mheshimiwa Mbunge, awahamasishe wananchi kama afanyavyo kila siku wa vijiji vya Kapalala na Kininga, vijiji ambavyo vilikuwa vinapata maji lakini mashine ikaibiwa wachangie gharama za kununulia mashine nyingine ili huu mradi uweze kufanya kazi na wananchi waweze kupata maji kama ilivyokuwa hapo awali. Aidha, wananchi wahamasishwe kuimarisha kamati za maji kwa lengo la kuimarisha ulinzi kwenye miradi yao ya maji. Hii ndiyo njia sahihi ya kumiliki na kuendesha miradi ya maji na kuifanya iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002, Serikali ina nia ya kuwapatia wananchi wake wote majisafi na salama ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo kasi ya usambazaji wa huduma ya maji itategemea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Kwa hali hiyo, vijiji nilivyovitaja na alivyovisemea Mheshimiwa Mbunge na vijiji vingine vyote hapa nchini vitaendelea kuhudumiwa kupitia kwenye Bajeti ya Serikali ya kila mwaka na kutokana na nguvu za wananchi wenyewe na wahisani mbalimbali.

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na kuhamasisha wananchi na pamoja na nguvu za Serikali kwanza naipongeza Wizara hii kwa kasi ya utendaji wake wa kazi. Lakini swali langu ni kwamba kwa nini kusiwe na jitihada maalum kama zile zinazofanywa na Wizara ya Elimu za MMEM kwa sababu suala la maji ni gumu? Vijiji hivi nilivyovitaja akina mama wanatoka asubuhi sana na wanarudi jioni hasa kiangazi na maji ni kidogo sana, je, Waziri anaweza kusaidia kama alivyosaidia vijiji hivyo vingine ambavyo amesaidia?

(b) Pamoja na mikakati iliyowekwa ya Sera ya Taifa, Serikali haioni kuwa sasa ingekuwa ni vizuri zaidi hii Sera ikatiliwa mkazo na ikaleta bajeti ambayo inge-sustain ingeweza kusaidia vijiji vingi kuweza kupata maji, vikiwemo Vijiji vya Kwajuni na Mwambani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Paul Ntwina, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi uwezo wa Serikali unategemea sana Bajeti yake. Lakini kwa bahati nzuri, baadhi ya vijiji katika Jimbo la Songwe vilipata usaidizi kutoka Serikali ya Denmark na tunaendelea kufanya hivyo kila nafasi inapopatikana. Lakini napenda nisisitize kwamba licha ya kwamba mpango wa elimu aliotolea mfano umefanikiwa, umefanikiwa kutokana na jitihada za wananchi wa sehemu hizo na walimu pamoja na wanafunzi kutunza miundombinu, au kutunza vifaa vya shule na kadhalika.

Sasa ikiwa miradi ya maji pia itatunzwa kwa mtindo ule ule tunaofanya kwenye shule za msingi, nina hakika miradi inayopelekwa vijijini itakuwa endelevu na itasaidia kupunguza matatizo ya maji. Lakini kama miradi hii itakuwa inahujumiwa kwa kuibiwa vifaa itakuwa ni vigumu sana tutakuwa tunapiga hatua mbili mbele tunarudi hatua tatu. Kwa hiyo, haitatufikisha kokote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Semanini na Moja Wegga. *(Kicheko)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniongezea namba ya jina hasa na kunipa nafasi ya swali la nyongeza. *(Makofi)*

Kwa kuwa Vijiji hivi vya Galula, Itindi, Fuko vinafanana na Vijiji hivi vya Mikumi na Kata ya Zomi. Pampu hizi zimeibiwa za shilingi milioni 60 tu na mabomba yaliyopo kule ni zaidi ya bilioni moja. Hivi kweli Serikali haina shilingi milioni 60 za kununulia injini za kufunga kwenye *machine* hizi? Ni kweli? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hatutakuwa na fedha za kukaa tunaweka pampu za shilingi milioni 60 zinaibiwa. Tutakapokwenda kununua tena kwa sababu ya *factor* ya *inflation* na mambo mengine ya mabadiliko ya fedha, haitakuwa shilingi milioni 60 tena, itabidi kutumia fedha nyingi zaidi. Kwa hiyo, la msingi ni kushirikisha wananchi wetu walio karibu na maeneo ya miradi hii wahusike katika kuitunza na kuilinda. Kwa eneo la Mikumi, sio bomba za maji tu na pampu za maji, hata reli za madaraja, zote utakuta mabomba yameibiwa. Kwa hiyo, utakuta mabomba yameibiwa. Kwa hiyo, utakuta kwamba hili tatizo nadhani kuna umuhimu wa kuliangalia kwa undani zaidi ili tuwarudishie mioyo shirikishi wananchi wetu ili wahusike katika kutunza miradi yetu ya aina yoyote ile ambayo inaletwa kwenye maeneo yetu.

**SPIKA:** Maswali kwa Wizara ya Kilimo na Chakula, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala.

Na. 389

**Ruzuku kwenye Mbolea**

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kutoa ruzuku kusaidia upatikanaji wa mbolea kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa:-

(a) Je, ni mafanikio yapi yamepatikana kutokana na mpango huo?

(b) Je, ni lini Serikali itapanua mpango huo kwa ajili ya nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika msimu wa mwaka 2003/2004 Serikali ilitenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwenda Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hadi mwezi wa Mei, 2004 shilingi bilioni 1.27 zilikuwa zimetumika. Mafanikio ya mpango huo yalikuwa kama ifuatavyo:-

(i) Tani 38,935 za mbolea zilipelekwa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mkoa wa Mbeya tani 14,016, Mkoa wa Iringa tani 14,955, Mkoa wa Ruvuma tani 8,771 na Mkoa wa Rukwa tani 1,193.

(ii) Katika Vituo Vikuu vya Kupokelea Mbolea vya Iringa, Makambako, Songea, Mbeya na Sumbawanga bei ya mfuko mmoja wa mbolea wenye kilo 50 uliuzwa kati ya shilingii 10,000/= na shilingi 14,000/= ikilinganishwa na bei ya wastani ya shilingi 16,000/= hadi shilingi 25,000/= kabla ya utaratibu wa fidia.

(iii) Katika msimu wa mwaka 2003/2004 matumizi ya mbolea katika Mikoa ya Nyanda za juu Kusini yaliongezeka kwa tani 7,500 ikilinganishwa na matumizi katika msimu wa mwaka 2002/2003.

(iv) Kumekuwapo na ongezeko la uzalishaji wa mahindi kutoka wastani wa tani moja kwa hekta kabla ya utaratibu wa fidia hadi wastani wa tani 2.5 kwa hekta katika msimu wa mwaka 2002/2003.

(b) Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Serikali imepanga kupanua utaratibu wa kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwa nchi yote. Ili kutekeleza mpango huo katika mwaka wa 2004/2005, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.24 kwa ajili hiyo.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Mbolea iko *exempted* na sio *zero rated* na kwa sababu hiyo *clearing agency* wanalipa *VAT,* wasafirishaji wanalipa *VAT,* lakini gharama hizi anazibeba mkulima kwa sababu muuzaji anayeuza Mbolea kwa mkulima hawezi kudai hiyo *VAT.*

Je, Serikali haioni kwamba ingekuwa jambo la busara kufanya mbolea kuwa *zero rated* badala ya kuwa *exempted* ili kumwondolea mkulima gharama za *VAT* anazozibeba kwa sababu ya kushindwa kudai hiyo *VAT?* *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa inaonekana kwamba ruzuku ya shilingi bilioni 1.27 ilifanya kazi lakini sio kwa mafanikio makubwa kwa mikoa minne, je, kwa kutenga shilingi bilioni 7.24 kwa nchi nzima na akasema ana mpango wa kueneza mpango huu kwa nchi nzima, haionekani wazi kwamba huu ni mchezo kwa sababu zinatakiwa zitengwe angalau shilingi bilioni 25 angalau kwa kuongelea nchi nzima? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ameshamaliza kuuliza swali lake la nyongeza. Sasa unakagua nini? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, suala hili la kodi kama alivyolielezea, kodi zote zinatazamwa upya kama alivyosema Waziri wa Fedha. Upo utaratibu, ikionekana kuna utata wa aina yoyote kama anaoueleza Mheshimiwa Mbunge, utashughulikiwa na taarifa tumepata tutashughulikia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili, kuhusu ruzuku aliyoitaja, sio kweli haikuwa na mafanikio. Katika jibu langu la msingi nimesema kuwa huko nyuma ongezeko la uzalishaji wa mahindi ulikuwa tani moja tu kwa hekta, lakini sasa ni 2.5. Haya ni mafanikio makubwa sana. Naomba Mheshimiwa Mbunge akiri hivyo kwamba ni mafanikio makubwa yaliyopatikana.

Sasa kuhusu ongezeko alilosema, anaona shilingi bilioni saba ni kidogo kuwa siyo pesa hizi peke yake zitakuwa zinahusika. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, alipokuwa anatoa hotuba yake alielezea vile vile kuwa *PEDEP* itahusika vile vile katika maeneo, vile vile aliongea juu ya *African Development Bank* imo katika miradi. Kwa hiyo, sio pesa hizi peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, ila sasa mafanikio ya haya yote yataweza kufanikiwa tu kama sisi Waheshimiwa Wabunge tutahusika sana katika kuimarisha zile Kamati za Kusimamia Utaratibu huu kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya na tutajaribu kutoa tena ile *circular* ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula kusudi wote tuhusike hasa katika kuandaa mahitaji halisi ya Mbolea katika maeneo yetu kusudi watu wasilalamike pakatokea mapungufu kama ilivyowahi kutokea mwaka huu, ulikuwa mwaka wa majaribio. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea kwa kuzingatia muda. Maswali kwa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Mheshimiwa Charles Kagonji.

Na.390

**Rushwa - Mahakama za Mwanzo**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi wananchi wa Tanzania moja kwa moja au kupitia Wawakilishi wao wamekuwa wakielezea usumbufu mkubwa, maonevu na rushwa iliyokithiri katika baadhi ya Mahakama zetu za Mwanzo ambazo nyingi ziko Vijijini ambako ndiko waliko wananchi wengi ambao wengi wao hawaelewi Sheria zinazowabana hata ule utaratibu wa kesi kwa ujumla haueleweki:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazomfanya mwananchi yeyote anayeweza kumudu huduma za Wakili katika Mahakama za Mwanzo asiruhusiwe kufanya hivyo?

(b) Je, kutomruhusu mwananchi kuchukua Wakili katika kesi za Mahakama za Mwanzo hasa ikizingatiwa ukubwa wa nchi yetu na umbali wa Mahakama za Wilaya kutoka zile za Mwanzo Vijijini sio kukiuka haki za msingi za binadamu?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mawakili wamekuwa hawaruhusiwi kutoa huduma zao katika Mahakama za Mwanzo kwa sababu nchi yetu ilipopata Uhuru haikuwa na wataalam wa sheria wa kutosheleza na hivyo Mahakama hizo za Mwanzo zikawa na Mahakimu wenye kiwango cha elimu ya chini tu cha sheria.

Katika mazingira kama haya Bunge kupitia Sheria ya Mahakama za Mahakimu ya mwaka 1963 na baadaye mwaka 1984 ilitunga Sheria ya Kuwazuia Mawakili wasitoe huduma zao katika Mahakama hizo kutokana na tofauti kubwa ya kiwango cha Elimu ya Sheria baina ya Mawakili na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali tayari imeshaanza kuajiri Mahakimu wenye kiwango cha Elimu ya Stashahada ya Sheria kuwa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo. Lengo la hatua hiyo ya Serikali ni kuwezeshwa Mawakili waanze kutoa huduma zao pia katika Mahakama za Mwanzo na hivyo kulinda haki za wananchi ipasavyo.

Hata hivyo kwa wakati huu mwananchi aliye na shauri katika Mahakama ya Mwanzo anayetaka kuwakilishwa na Wakili katika shauri lolote linalomhusu, anayo haki ya kuomba shauri lake lihamishiwe katika Mahakama ya Wilaya ili Wakili wake amwakilishe katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kesi za madai katika Mahakama za Mwanzo wahusika wana haki ya kuwakilishwa na mmoja wa jamaa au mwanafamilia ilimradi asiwe mwanasheria.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumtaarifu Mheshimiwa Charles Kagonji, kwamba hivi sasa Tume ya Kurekebisha Sheria imekamilisha taarifa yake ya mwisho juu ya uwezekano wa kuwaruhusu watu wasio Wanasheria lakini wanazielewa sheria zetu *(paralegal)* ili waweze kuwawakilisha wananchi wenye kesi katika Mahakama za Mwanzo.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Hata hivyo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

La kwanza, hivi kwa sababu suala la rushwa katika Mahakama zetu za Mwanzo limelalamikiwa mara nyingi sana na wananchi wenyewe na hata kupitia kwa Wawakilishi wao. Hivi kwa malalamiko hayo, Serikali ina mkakati gani wa kulishughulikia suala hilo katika ngazi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili angalau rushwa iweze kupungua katika maeneo hayo? Maana kwa kweli ni kero kubwa sana.

Pili, hivi Wizara hii kwa sababu suala hili ni kubwa na ni kero kwa nchi nzima, imejaribu kufanya utafiti? Kama bado itafanya utafiti ili kujua hasa kwa nini suala hili linaendelea kuwa kero kubwa? Ni matatizo ya wananchi wetu kutoelewa haki zao? Ni Mahakimu hawa kuwa na njaa au mishahara midogo au ni tatizo gani? Tunaomba majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli na humu ndani ya Bunge tumekuwa tukikiri kwamba lipo tatizo hili la rushwa na limekuwa likizungumziwa na kuandikiwa hoja katika ripoti mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ripoti ya Warioba kuhusu suala la rushwa. Pia Mheshimiwa Wilson Masilingi, ametoa mikakati ya Kitaifa kuhusu jinsi ya kutatua tatizo hili. Lakini niseme kwa upande wa Idara ya Mahakama pia sisi tunayo mikakati kuhusiana na kero hii.

Kwanza kwa miaka yote hii ambapo mimi nimekuwa ni Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na walionitangulia na watakaokuja, tumekuwa tukiwasimamisha Mahakimu ambao wanabainika kwamba wanajiingiza kwenye vitendo hivi vya rushwa, baadhi wamepelekwa Mahakamani, wengine wamefungwa na wengine wamefukuzwa na wengine wamesimamishwa.

Vile vile tumeunda Bodi za Mahakama kushughulikia masuala haya, tunazo Kamati za Maadili katika Mahakama yenyewe kuweza kuwachunguza na tumekuwa tunaboresha mishahara ya Majaji, Mahakimu na Makarani ili wasipate hiyo *temptation* ya kujihusisha na masuala ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, pia tumeweka mkazo katika suala la ukaguzi, kuzikagua Mahakama zetu mara kwa mara. *(Makofi)*

Suala la utafiti, nadhani ni kutokana na utafiti huo wa kero na sababu za rushwa ndio maana tumeweza kuwa na mikakati kama hii.

**SPIKA:** Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Maria Watondoha.

Na. 391

**Ujenzi wa Barabara**

**MHE. MARIA D. WATONDOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati Serikali ilipokuwa ikijibu swali Na.210 tarehe 12 Julai, 2002 ilieleza kwamba Serikali inao wajibu wa kujenga barabara lakini haina uwezo wa kutosha na kwa kuwa kuwa na barabara nzuri kunasaidia kukua kwa uchumi kwani maeneo mengi yanaweza kupitika kwa urahisi:-

(a) Kama Serikali haina uwezo, kwa nini isitumie mfumo wa *BOT?*

(b) Je, kwa Serikali kuchelewa kufanya uamuzi wa kujenga barabara kwa mfumo wa *BOT* au *BOOT* haioni kwamba tunazidi kurudi nyuma kimaendeleo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *BOT* ni mfumo unaoruhusu wawekezaji binafsi kujenga barabara au madaraja kwa fedha zao na kutoza ushuru kwa watumiaji wa miundombinu hiyo hadi hapo watakaporudisha gharama na hatimaye kuirejesha miundombinu hiyo Serikalini. Mfumo huu ni mzuri hasa ikizingatiwa kwamba nchi yetu haina uwezo wa kutosha kuweza kujenga barabara na madaraja yote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua manufaa yanayotokana na mfumo huu wa kujenga barabara ambayo ni njia mojawapo ya mageuzi ambayo inaweza ikaleta manufaa kwa Taifa katika Sekta ya Barabara. Manufaa hayo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kupunguza mzigo kwa Serikali wa kutegemea Bajeti;

(ii) Kupunguza utegemezi kwa Wafadhili; na

(iii) Kuongeza uwezo wa kujenga barabara katika maeneo ambayo yangechukua muda mrefu kabla ya kupata huduma za barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa *BOT* bado si njia pekee ya kuondoa matatizo ya barabara na ndio maana Serikali imekuwa ikitumia njia mbalimbali ikiwemo *special project, road fund money,* fedha za wafadhili na kadhalika katika kuhakikisha barabara zinatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, sio kweli kuwa Serikali imechelewesha kufanya uamuzi wa kujenga barabara kwa mfumo huu. Tangu mwezi Februari, 2003, Serikali imekwishapitisha Sera ya Taifa ya Sekta ya Ujenzi. Mojawapo ya maeneo muhimu yanayoainishwa katika sera hii ni ujenzi wa barabara kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa kutumia mifumo mbalimbali kama *Build-Operate-Transfer (BOT), Build -Own-Operate-Transfer (BOOT), Design-Build-Finance-Operate (DBFO)* na kadhalika. Hivyo, kama Mheshimiwa Maria Watondoha, anao au amewapata wawekezaji wanaotaka kujenga barabara zetu kwa njia ya *BOT,* wanakaribishwa ili tushiriki nao katika kuendeleza jambo hili muhimu kwa Taifa.

Aidha, Wizara yangu itaendelea kufanya majadiliano na wawekezaji wengine wenye nia nzuri ya kujenga barabara au madaraja kwa mfumo huu ili kuongeza mtandao wa barabara zetu ambazo ni muhimu katika kuinua uchumi wa nchi.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri anasema upo mfumo mbadala ambao ni *special projects* kama barabara za lami zinazojengwa kutoka Dodoma kwenda Manyoni, Singida na barabara ya lami kutoka Dar es Salaam, Kibiti Lindi, kwa kuwa barabara hizi za *special projects* zinaunganisha Mikoa tu na zinajengwa kwa kiwango cha lami, kwa kuwa barabara ambazo zinajenga uchumi ni zile za Vijijini na zinajengwa kwa kiwango cha udongo tu, je, Serikali haioni wakati umefika sasa kutenga fedha za kutosha kuweza kujenga barabara hizi zinazounganisha Wilaya katika kiwango cha lami? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa katika jibu la msingi vile vile Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sera toka mwaka 2003 imeruhusu mfumo wa *BOT* au *BOOT* au *DBFO,* je, Serikali imepata wawekezaji wangapi katika utaratibu huo kwa kuzingatia sera zetu pamoja na jitihada za Wabunge ambazo ametuagiza sasa? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Maria Watondoha, kwamba Serikali itakapopata rasilimali za kutosha, ni vyema vile vile barabara zinazounganisha Wilaya zijengwe kwa njia ya lami. Subiri tuongee tuendelee kupata rasilimali za kujenga barabara hizo.

Pili, kuhusu suala la *DBFO* na *BOOT,* kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, nimemwomba Mheshimiwa Maria Watondoha, kwamba kama atapata wawekezaji wanaotaka kutumia utaratibu huo, basi awalete tushirikiane nao. Kwa maana hiyo ni kwamba bado hatujapata wawekezaji. Lakini kati ya barabara ambazo zinafikiriwa kufanyiwa utaratibu huo, ni barabara ya Mtwara, Masasi, Songea na *Mbamba Bay,* daraja la Umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, daraja la Kigamboni, barabara ya Manyoni - Itigi - Tabora na Kigoma na barabara nyingine bado zinaainishwa kuingizwa katika utaratibu huo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Maswali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Na. 392

**Askari wa Usalama Barabarani**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Je, ni *Traffic Police* wangapi wamepatwa na majanga ya kugongwa au kugonjwa na kufa wakiwa katika kazi zao za kuongoza magari na kusimamia masuala ya usalama barabarani kwenye barabara mbalimbali hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1999 hadi Juni, 2004 jumla ya askari wanane wa Usalama Barabarani walikumbwa na mjanga ya kugongwa na kufa wakiwa katika kazi za kuongoza magari na kusimamia masuala ya usalama barabarani kwenye barabara mbalimbali hapa nchini. Kati ya matukio hayo manane, matatu yaliwahusu askari wapanda pikipiki ambao walikuwa katika doria za kawaida.

Aidha, askari 15 wamejeruhiwa wakiwa katika kazi zao za kuongoza magari na kusimamia misafara ya viongozi hapa nchini. Kati ya hao 15 waliojeruhiwa kumi walikuwa wapanda pikipiki na watano walikuwa katika kazi za kawaida za kuongoza magari.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa sehemu nyingi hasa katika Jiji la Dar es Salaam zinaongozwa na zile taa ambazo zinaendeshwa kwa teknolojia ya kisasa, *computer* na papo hapo yanaongozwa na matrafiki kitendo ambacho kinasababisha ku-*confuse* hata madereva wengine na kusababisha matrafiki hao kugongwa, je, Serikali inalionaje suala hili na kulipatia ufumbuzi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa mahali kama Dar es Salaam ni msongamano wa magari na vurugu sio taa wala sio *traffic,* tatizo kubwa la Dar es Salaam pale ni magari yanaongezeka sana, barabara nyingi ni zile zile, ni nyembamba, hapo ndipo penye tatizo. Kuna wakati baadhi ya watu kule Dar es Salaam, hata baadhi ya Wabunge walifikiri pengine *traffic* ndilo tatizo.

Kuna siku moja nadhani wengine mnakumbuka Dar es Salaam mwaka 2003, *Traffic Police* wote hawakwenda kwenye barabara, siku hiyo zikaachiwa tu taa zifanye kazi. Sasa vurumai iliyokuwepo siku hiyo, Waziri wa Mambo ya Ndani alipata simu zaidi ya 50 na *IGP* naye simu zaidi ya 50 wakiomba kwamba sasa *traffic* warudi barabarani. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, nasema tatizo kubwa pale ni barabara. Lakini bahati nzuri Wizara ya Ujenzi waliwahi kutoa ripoti hapa kwamba wanao mpango wa kupanua barabara Dar es Salaam na kujenga zile barabara za juu kwa juu, *flyovers.* Hatua hiyo ikifikiwa, malalamiko ya Dar es Salaam yatapungua sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bado ninayo maswali mawili, ni bora yapewe nafasi. Maswali kwa Wizara ya Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Esha Stima.

Na.393

**Malalamiko ya Walimu Daraja la IIIA na IIIB**

**MHE. ESHA H. STIMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna malalamiko mengi kutoka kwa baadhi ya Walimu wa Daraja la *IIIB* walioanza kazi mwaka 1994 Julai na Daraja la *IIIA* waliojiendeleza kuwa hulipwa mishahara midogo hata kama wamejiendeleza na kupata Vyeti vya kufaulu Kidato cha Nne kama Wizara ilivyoagiza Walimu wake kujiendeleza:-

Je, Walimu wa madaraja hayo *(IIIB* na *IIIA)* wanastahili kulipwa mishahara kiasi gani na katika kima gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA - k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Esha Stima, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu wa zamani, Mwalimu wa Daraja la *IIIB* aliyetaka kujiendeleza alitakiwa kusoma kwanza masomo ya taaluma ili kufikia kiwango cha Elimu ya Kidato cha Nne. Baada ya hatua hiyo, Mwalimu mhusika alijiunga na Chuo cha Ualimu na kusomea Mafunzo ya Ualimu Daraja la A. Baada ya kufaulu na kupata Cheti ndipo alibadilishiwa muundo wa utumishi wake kuwa Mwalimu wa Daraja la *IIIA* la kusomea. Hivyo, kwa kufaulu Kidato cha Nne peke yake Mwalimu wa Daraja la *IIIB* alikuwa hapandishwi kuwa Mwalimu Daraja la *IIIA* mpaka akachukue mafunzo ya Elimu ya Ualimu wa Daraja la *IIIA* na kufaulu mtihani husika. Lakini sasa umeanzishwa utaratibu mpya wa Daraja *IIIA* kazini ambao haupitii Kidato cha Nne wala Chuo cha Elimu ya Ualimu, bali Mwalimu wa Daraja la *IIIB* na *IIIC* ananolewa katika masomo anayojifundisha na akifaulu masomo hayo manne kwa alama ya “B” katika mtihani unaofanana na wa Darasa la Saba lakini sio wa Darasa la Saba, anapandishwa kuwa Daraja la *IIIA* kazini. Utaratibu huu utawaboresha Walimu katika kuyajua na kufundisha masomo ya Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Esha Hassan Stima, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.10 wa mwaka 2002 kuhusu miundo ya Utumishi wa kada zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni, Walimu wa Daraja la V yaani C na B na Daraja la IV au *IIIA,* wameunganishwa kuwa Walimu Daraja la III katika ngazi ya Mshahara *TGTS B.*

Aidha, kwa mujibu wa Waraka wa Watumishi wa Serikali Na.2 wa mwaka 2004 kuhusu mabadiliko ya mishahara ya kuanzia miundo ya ngazi za mishahara ya Watumishi

wa Serikali, kuanzia tarehe Mosi Julai, 2004 mshahara wa kuanzia Mwalimu wa Daraja la *IIIB* ni shilingi 87,090/= kwa mwezi na mshahara wa kuanzia Mwalimu wa Daraja la *IIIA* ni shilingi 88,970/= kwa mwezi. Kwa hiyo, mishahara wanayostahili kulipwa Walimu hao inategemea jinsi walivyopanda vyeo baada ya kuanza kazi.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini bado nina swali dogo la nyongeza. Nilikuwa nauliza hivi lini Wizara ya Elimu na Utamaduni itaweka utaratibu wa kutoa mafunzo au Semina kuwaelimisha walimu ili waweze kujua haki zao ambazo baadhi yake amezijibu katika swali langu ili kuondoa malalamiko na usumbufu kwa walimu nchi nzima? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA - k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimshukuru Mheshimiwa Esha Stima, kwa swali lake, maana kanuni zetu zinasema, swali lengo lake ni kutaka kupata taarifa au hatua ichukuliwe jambo fulani litekelezwe. Kwa kuwa anachokiuliza ni elimu kwa walimu ili wajue haki zao, kama tulivyotaja katika majibu ya swali la msingi, mimi nina hakika Wizara ya Elimu na Utamaduni italifanya hilo kwa niaba na faida ya Walimu kama sehemu muhimu ya wanajamii wetu.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa leo, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa.

Na.394

**Malipo ya Mkupuo**

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mkutano wa Bunge wa Bajeti wa mwaka 2002/2003, Wabunge wengi walilalamikia uamuzi wa Serikali wa kulipa malipo ya mkupuo kwa wastaafu na kwa kuwa utaratibu huo umesababisha kero na adha kubwa kwa wazee wetu na hata vifo na kwa kuwa Serikali ilitoa tamko kuwa italifanyia kazi tatizo hilo kabla ya mwezi wa Desemba, 2003 na kwa kuwa wazee hao wana hamu ya kujua hatima ya tatizo hilo na uamuzi wa Serikali:-

(a) Je, nini tamko la Serikali juu ya kuondoa kero hiyo kwa wastaafu ambao wameitumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa?

(b) Je, ni wastaafu wangapi (idadi yao) ambao wameathirika na tatizo hilo la mkupuo nchini kote?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba kwanza nitoe maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kulipa pensheni kwa mkupuo ulifuatia maombi ya wastaafu wenyewe kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kiwango kidogo cha pensheni ya kila mwezi. Lengo lilikuwa ni kuwaondolea adha na kero ya kufuatilia pensheni hizo na gharama kubwa za usafiri, malazi na kadhalika. Aidha, kama nilivyosema wakati najibu swali Na. 4 la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, katika Mkutano huu wa Kumi na Sita wa Bunge, baadhi ya wastaafu walikuwa na malengo ambayo yalihitaji fedha nyingi kwa wakati mmoja. Hivyo, kuchukua pensheni kwa mkupuo ilikuwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na makali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema jana kwenye hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2004/2005, Serikali ilikwishaamua kuwarejesha wastaafu waliochukua pensheni yao kwa mkupuo katika daftari la pensheni ya kila mwezi. Hivi sasa Serikali inaandaa mazingira mazuri ya utekelezaji wa azma hiyo, ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya sheria na kanuni zilizoruhusu malipo hayo ya mkupuo.

Aidha, Serikali pia inafanya zoezi la kuwatambua wastaafu nchini kote ili kupata idadi yao kamili kwa ajili ya kuepuka kuwalipa wastaafu hewa au wasio waaminifu. Zoezi hilo linatarajiwa kukamilika mwisho wa mwezi Agosti, 2004 na malipo ya kwanza yatafanyika mwezi Januari, 2005 baada ya kukamilisha taratibu zote.

(b) Mhehsimiwa Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu tulizo nazo, idadi ya wastaafu waliokumbwa/waliofaidika na zoezi la kulipwa mkupuo ni 35,000. Hata hivyo idadi halisi itajulikana baada ya zoezi la kuwatambua kukamilika.

**SPIKA:** Kwa kuwa swali ni la zamani pengine hakuna maswali ya nyongeza. Analo swali la nyongeza.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na kwamba swali langu ni la muda mrefu. Lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nilikuwa na swali moja dogo tu la nyongeza, kwamba toka Serikali imefanya uamzi huo wa kuwarejesha hawa wastaafu kwenye pensheni, Serikali inakumbana na matatizo gani katika kuwasajili upya hawa wastaafu kwa sababu inavyoonekana ni kwamba taarifa hazijawafikia baadhi ya wastaafu ambao wako kwenye maeneo ambayo si ya mjini hasa wale wanaoishi vijijini. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba taarifa zinawafikia wastaafu ambao wako mbali na *centers* hizi za mjini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, tatizo la taarifa sidhani kwamba kuna wananchi wanaohusika katika zoezi hili ambao hawajapata taarifa. Tunaamini matangazo yamekuwa yanatolewa kwa muda mrefu kuanzia ngazi ya Taifa mpaka ngazi ya kijiji wana taarifa. Tatizo kubwa linalokabili zoezi hili ni kutokupata kwa baadhi ya kumbukumbu za kuonyesha kwamba

wao wanahusika na zoezi hili. Kuna wengine barua za kumbukumbu za kustaafu hazionekani, wengine hawana vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ama Wizara ya Fedha iliweka utaratibu wa watumishi kutoka Hazina kwenda kila Wilaya, pia Ofisi ya *TRA* na wahusika walialikwa waende pale ili waweze kutambuliwa na wale ambao walikuwa na upungufu wa vitambulisho au nyaraka za kuwathibitisha kwamba ni wahusika basi utaratibu ulikuwa unafanywa kwa ajili ya kuwasiliana na Wizara ya Fedha pamoja na sehemu walizokuwa wanafanyia kazi kuhakikisha kwamba hao ndio wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana zoezi la kuwalipa inabidi lisubiri mpaka tutakapojiridhisha kwamba watu watakaolipwa ni wahusika ili tuweze kuwaondoa matapeli wale ambao sio waaminifu wasiweze kulipwa fedha hizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yote ya msingi yamejibiwa. Sasa matangazo ya vikao vya leo. Leo Kamati tano za kudumu zimejipangia vikao na kwani tunakaribia kumaliza *session* basi wanatakiwa wamalize viporo vyote vilivyobaki.

Kamati za Kudumu ya kwanza ni Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa Dr. John Malecela, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anaomba Wajumbe wakutane saa 10.00 jioni leo tarehe 5 Agosti, 2004 katika chumba namba 231 ghorofa ya pili. Ni Kamati ya Ulinzi na Usalama saa 10.00 jioni chumba namba 231.

Kamati ya pili ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti Mheshimiwa Sophia Simba, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 5 Agosti, 2004 katika chumba namba 227, ghorofa ya pili kuanzia saa 5.00 asubuhi hii. Kamati ya Maendeleo ya Jamii saa 5.00 asubuhi chumba namba 227.

Kamati ya tatu ni Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. William Shija, anawaomba Wajumbe wakutane saa 5.00 asubuhi katika chumba namba 219 ghorofa ya pili, Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, saa 5.00 asubuhi chumba namba 219.

Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shellukindo, anawaomba Wajumbe wa Kamati wakutane leo tarehe 5 Agosti, 2004 saa 5.00 asubuhi chumba namba 231, Uwekezaji na Biashara saa 5.00 asubuhi chumba namba 231.

Kamati ya mwisho ni Kamati ya Miundombinu, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Henry Shekiffu, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Miundombinu wakutane saa 5.00 asubuhi hii chumba namba 428 ghorofa ya nne. Hizo ndizo Kamati ambazo zinakutana leo.

Isiyokuwa Kamati ya Bunge ni Chama Cha Wabunge Vijana, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, anawaomba Wabunge wote vijana wakutane katika kikao

kifupi saa 7.00 mchana. Chumba namba 132 ghorofa ya kwanza. Mwisho wa matangazo. Katibu tuendelee na *Order Paper.*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Ngoja, Miswada hii yote miwili itasomwa Mara ya Kwanza, halafu ndiyo tutarudi hatua ya kusoma Mara ya Pili, Muswada mmoja mmoja. Kwa hiyo, Katibu sasa isome yote miwili kusomwa mara ya kwanza.

**Muswada wa Sheria ya Serikali Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2004**
***(The Appropriation Bill, 2004)***

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka Wa mwaka 2004**
***(The Finance Bill, 2004)***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Serikali wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali Mwaka 2004**
***(The Appropriation Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria kutumia shilingi 2,866,364,083,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kwa kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2004/2005 nilieleza shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 2,866.364,083,000/= kwa mwaka 2004/2005 kama ifuatavyo: Kwanza matumizi ya kawaida shilingi 1,774,773,493,300/=, pili, matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 1,091,590,589,700/= na jumla ni shilingi 2,866,364,083,000/=.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekwishajadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri wakati wakiwasilisha Makadirio ya Wizara zao. Madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Serikali ya mwaka 2004/2005 ya jumla ya shilingi 2,866,364,083,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo yaliyokubaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naomba kutoa hoja.

**MHE. HARITH B. MWAPACHU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Utaratibu wa kushughulikia Miswada hii inayoitwa *Appropriation Bill* ni tofauti na Miswada ya kawaida. Nikumbushe tu kwamba huko kwenye Kanuni zetu Na. 81 (vii) inasema baada ya Bunge kukamilisha kazi yote ya kufikiria Makadirio ya Matumizi ya Wizara zote kwa mwaka unaohusika kazi ambayo tuliimaliza jana ule Muswada wa Fedha za Matumizi utawasilishwa Bungeni ndiyo huu. Utawasilishwa Bungeni na kupitishwa kwa mfululizo katika hatua zake zote.

Muswada wa aina hii hautapelekwa katika Kamati inayohusika, wala Kamati ya Bunge Zima, ndiyo utaratibu wenyewe. Kwa hiyo, kwa kufuata utaratibu huo sasa tuujadili. Sijapata maombi yoyote, nina maombi mawili. Niletee, niletee. *(Makofi)*

Kuna maombi mawili yalishapita kwa Makatibu Mezani. Kwa kuwa hawakuleta kwenye Kamati hakuna maoni ya Kamati, wala ya Upinzani. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, atafuatiwa na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa na ndiyo wawili tu waliojiandikisha.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja iliyoko mbele yetu na nakubaliana kabisa na hii hoja. Lakini hizi fedha zinapokwenda kwenye miradi ya maendeleo au matumizi ya kawaida katika mzunguko wake na kuwafikia wananchi, kuna malalamiko kwamba hizi fedha zinapowafikia wananchi kuna fedha shilingi 100 na shilingi 50, hizi zinawapa tabu sana huko vijijini, wanakataa wafanya biashara kupata huduma wananchi. Kwa sababu hizi shilingi 100 na shilingi 50 sijui *material* yake ikoje, zingine zinakuwa zimetobokatoboka, zingine sura ya Mwalimu inakuwa haionekani.

Siku moja nilishaitwa na mpigakura wangu mmoja mzee, akaniambia unaona giza kabisa ndani humu na hela ninazo hizi shilingi 150/= wamekataa dukani kule kwa sababu hizi hela zimetobokatoboka. Sasa kamwambie Waziri huyo afanye taratibu wa kubadilisha shilingi 100/= na shilingi 50/= shilingi 200/= haina matatizo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hilo tu kuufikisha ujumbe niliotumwa na wapigakura wangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba hizi fedha za shilingi 100/= na shilingi 50/= zinawapa matatizo huko vijijini, zinakataliwa wanapopata huduma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa! Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, ameshaingia mitini. *(Kicheko)*

Kimbia basi Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, nakuona. Unaweza kuchangia Mheshimiwa Mgaywa.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi sikujua kama ningekuwa wa pili. Nashukuru kwa hoja hizi zote mbili.

**SPIKA:** Ah! Ni moja tu tunayoijadili sasa *Appropriation Bill,* yenye rangi hii inaidhinisha tu matumizi ambayo tumeshayakubali katika Bunge hili. Endelea. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba hoja ipite kama ilivyopangwa, tupate hela. Lakini ningeomba niongezee jambo moja kwamba katika Bajeti itakayokuja namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie uwezekano sasa wa kuwezesha majimbo kufanya kazi, kwa maana kwamba kufanya kazi kwa maana kwamba pesa tunapoomba sisi Waheshimiwa Wabunge kuna vijambo vidogo vidogo kama barabra, maji, ambayo yanahitaji shilingi milioni 20, 30. Sasa kutengwe bajeti ndogo inaenda moja kwa moja jimboni na Mheshimiwa Mbunge awe Mwenyekiti wa kuratibu matatizo madogo madogo halafu ile bajeti iende moja kwa moja asianze kuhangaika na mambo madogo madogo ya kuleta Bungeni, ili tumpunguzie mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba nitoe majibu kwa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Abdillahi Namkulala na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa.

Kwanza suala la shilingi 50/= na shilingi 100/=, Mheshimiwa Waziri wakati wa Bunge hili la Bajeti alitolea kauli na alisema kwamba ameshaagiza Gavana wa Benki Mkuu kuliangalia suala hili ili kurekebisha, kwamba kuhakikisha hizi fedha zitakazotolewa za shilingi 50/= na shilingi 100/= hazina matatizo kama ilivyo hivi sasa. Kwa sababu imeshatolewa lakini bado hatua zake zinazohusika zinachukuliwa na Benki Kuu.

Kuhusu suala la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, kila mwezi Wizara ya Fedha inapotoa fedha kwenda huko Wilayani na Mikoani huwa inatangaza katika magazeti fedha kiasi gani zinakwenda huko.

Ni matumaini yetu kwamba Waheshimiwa Wabunge wote fedha zile zinazokwenda kwa ajili ya huduma mbalimbali, za barabara, za maji, kilimo na wengine, wanaweza kuzifuatilia na kuhakikisha kwamba katika Halmashauri ambazo wao ni Madiwani vile vile wanahakikisha fedha zile zinatumika kama ilivyokusudiwa na wao wahakikishe kwamba fedha zile zinatumika kwa ajili ya jambo lile au *project* ile inayokusudiwa na washirikiane vya kutosha katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuifanyie uamuzi hoja hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Bungeni Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Hatua hiyo imekamilika, Mheshimiwa Waziri toa hoja kwamba Muswada sasa usomwe Mara ya Tatu.

**Muswada wa Sheria ya Serikali wa Kuidhinisha Matumizi ya Serikali Mwaka 2004** ***(The Appropriation Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa kutumia fedha shilingi 2,866,364,083,000/= toka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Hoja hiyo nayo imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, nayo ni kwamba, Muswada huu sasa ukubaliwe. Wote wameafiki, Muswada wa *Appropriation* wa mwaka 2004 umekubaliwa na Bunge. Sasa utakwenda kwa Rais kupata idhini yake. *(Makofi)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2004**
***(The Finance Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Namwita mtoa hoja. Niwataje waliojiandikisha kuchangia Muswada huu ili waanze kujiandaa. Ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdulatif Esmail,

Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa tena na Mheshimiwa Philip Marmo. Hao ndio wameshajiandikisha mpaka sasa. Orodha haijafungwa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2004 *(The Finance Bill, 2004),* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ambao ni utekelezaji wa maamuzi ya Bunge kuhusu hoja za Bajeti ya mwaka huu wa fedha unakusudia kuzifanyia marekebisho Sheria 13 zifuatazo:-

(i) Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972;
(ii) Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 1970;
(iii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 332;
(iv) Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003;
(v) Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995;
(vi) Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004;
(vii) Sheria ya Vileo ya mwaka 1968;
(viii) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982;
(ix) Sheria ya Hitimisho ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999;
(x) Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1972;
(xi) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya mwaka 1997;
(xii) Sheria ya Mafunzo ya Ufundi Stadi ya mwaka 1994; na
(xiii) Sheria ya Rufani za Kodi ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu 14. Sehemu ya kwanza inahusu mambo ya utangulizi. Sehemu ya pili inafanyia marekebisho Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1972 kwanza kwa kurekebisha kifungu cha tatu cha Sheria hiyo ili leseni ya biashara iwe inatolewa mara moja tu wakati biashara inapoanzishwa isipokuwa tu pale ambapo kutakuwa na mabadiliko ya biashara kama vile ongezeko la mapato yaani *turn over* kuzidi shilingi milioni 20 kwa mwaka. Kufutwa kwa leseni au kufungwa kwa biashara.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kupunguza mzigo wa kodi na ada kwa walipa kodi na kuboresha mazingira ya biashara.

Pili, kurekebisha kifungu cha nane cha sheria hiyo ili kufuta ada ya leseni inayotozwa kwa biashara zenye mapato yasiyozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka.

Biashara hizi zitapewa leseni bila kulipia ada. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama na kuwezesha vijana na wafanyabiashara wadogo kuanzisha biashara kwa njia halali.

Tatu, kufanya marekebisho katika kifungu hicho cha nane ili biashara zenye mapato ya shilingi milioni 20 na zaidi kwa mwaka zitozwe ada ya leseni ya shilingi 20,000 tu ili kupunguza gharama zinazoambatana na kuanzisha biashara na kuweka mazingira mazuri ya kuingiza biashara nyingi katika uchumi rasmi.

Nne, kufuta ada za leseni zinazotozwa chini ya kifungu cha nane cha Sheria hii, pale ambapo biashara husika inasimamiwa chini ya Sheria nyingine za kisekta ambapo leseni nyingine hutolewa chini ya sheria hizo.

Tano, kufuta kifungu cha tisa cha Sheria hiyo ya 1972 ili kufuta ada za biashara kwa hospitali, zahanati na vituo vya afya vinavyomilikiwa na kuendeshwa na madhehebu ya dini. Hatua hii ina lengo la kupanua na kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Mwisho kwa kurekebisha kifungu hicho cha tisa, kwa kuweka majedwali mawili yenye sehemu (a) na (b) ili kuainisha mamlaka zitakazokusanya ada za leseni kwa biashara mbalimbali yaani Serikali Kuu na Serikali za Mitaa tofauti na ilivyo sasa ambapo mchanganuo huu haukuwekwa bayana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu inapendekeza kufanyia marekebisho sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki, Sura ya 27 ya mwaka 1970 katika vifungu vya 48, 53, 154 na 178 kama ifuatavyo:-

(a) Kuweka utaratibu madhubuti wa kushughulikia mizigo inayohifadhiwa katika maghala ya Forodha kwa kuongeza kiwango cha riba kwa mizigo itakayohifadhiwa katika maghala kwa muda wa zaidi ya miezi mitatu ili viwango hivyo viende sambamba na viwango vya riba vya mikopo vinavyotozwa na mabenki ya biashara.

(b) Kuongeza viwango vya adhabu kwa wenye maghala ya forodha wanaotumia maghala hayo bila kuwa na leseni na kwa wenye maghala ambao tayari wamepewa adhabu ya malipo na kuendelea kuzembea kulipa adhabu hiyo.

(c) Kuondoa ushuru wa bidhaa kwa vifaa yaani *parts* na mashine vitakavyoingizwa nchini kwa shughuli za kilimo kama vile *windmills.*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nne ina lengo la kufanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 332 katika vifungu vya tatu, nne, kumi, 20 pamoja na jedwali la kwanza. Katika sehemu hii inapendekezwa:-

(a) Kuweka ushuru wa bidhaa yaani *Excise Duty* kwenye huduma ya *Television* ya kulipia yaani *Pay to view TV* kupitia *satellite* kwa kiwango cha asilimia 5 isipokuwa kwa huduma zitolewazo na Serikali au Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji.

(b) Kuruhusu Sheria ya Ushuru wa Bidhaa kutumika katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano badala ya utaratibu uliopo hivi sasa ambapo ushuru huo hukusanywa Tanzania Bara pekee. Aidha, chini ya utaratibu huu mapato yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kwa upande wa Tanzania Zanzibar yatabaki huko huko Tanzania Zanzibar.

(c) Katika jedwali la kwanza kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi, mvinyo, vinywaji vikali, sigara na tumbaku, ili vilingane na hali halisi ya mfumko wa bei. Katika eneo hili inapendekezwa mvinyo utakaotengenezwa kutokana na Zabibu za hapa nchini usitozwe ushuru wa bidhaa. Lengo ni kupanua soko la zabibu zinazolimwa hapa nchini ili kupanua kilimo cha zao hilo hasa hapa Mkoani Dodoma.

(d) Kupunguza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwa vinywaji baridi kutoka shilingi 40/= kuwa shilingi 39.4. Hatua hii imechukuliwa baada ya kutafakari maoni ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa hotuba ya Bajeti.

(e) Kuondoa ushuru wa bidhaa kwa gesi ya Songo Songo ambayo imeanza kutumika hivi karibuni. Hatua hii itawezesha kuwa na umeme wa uhakika kutokana na *TANESCO* kuanza kutumia gesi hiyo kuzalishia umeme.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tano inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Michezo ya kubahatisha ya mwaka 2003. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza tafsiri ya baadhi ya maneno na kufanya marekebisho ya kiujumla ya vifungu mbalimbali yahusuyo sheria ya zamani ya Kodi ya Mapato ili viende sambamba na vifungu vya Sheria mpya ya Kodi ya Mapato ya Mwaka huu wa 2004.

Mheshimiwa Spik,a inapendekezwa pia kuongeza adhabu kwa wanaokwepa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria hii ili adhabu ziende sambamba na adhabu zitolewazo chini ya Sheria mpya ya Kodi ya Mapato. Sehemu ya sita inakusudia kurekebisha Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995 kwa kujumuisha ada mbalimbali za *visa* na kupunguza viwango vya ada hizo kwa kutoza ada ya dola za Kimarekani 100 kwa *multiple visa* za zaidi ya miezi sita na dola 50 kwa multiple *visa* za miezi sita na chini ya miezi sita na pia kwa aina nyingine zote za *visa.* Pendekezo hili lina lengo la kuvutia watalii na wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Sehemu ya saba inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kama ifuatavyo:-

(a) Kufanya marekebisho katika jedwali la tatu na baadhi ya vifungu ili kutoa unafuu wa asilimia 100 yaani *100% expensing* ya gharama za mtaji katika mwaka wa kwanza wa kutumia rasilimali katika sekta ya kilimo, misitu, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, unafuu huu pia utahusu mitambo ya usindikaji wa samaki na mazao ghafi ya kilimo. Aidha, pamoja na unafuu huu kifungu Namba 19 kinafanyiwa marekebisho ili kutoa tahadhari kwamba unafuu unaotolewa usitumike vibaya bali

utumike kwa sekta ya kilimo tu. Nikimaanisha mazao, samaki, mifugo na asali na pia kufafanua kwa kina maana ya biashara ya kilimo.

(b) Kufanya marekebisho ya kiuandishi chini ya kifungu Namba 142 ili kufafanua tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii.

(c) Kwenye jedwali la kwanza inapendekezwa kurekebisha viwango vya kodi kwa wafanyabiashara wadogo wanaotunza kumbukumbu na wale wasiotunza kumbukumbu. Lengo ni kuwapunguzia kodi wafanyabiashara wanaotunza kumbukumbu na hivyo kuhimiza wafanyabiashara wadogo kujenga tabia ya kutunza kumbukumbu za biashara zao.

(d) Kufanya marekebisho katika jedwali la kwanza ili kuongeza kiwango cha chini cha mapato ya wafanyakazi na wafanyabiashara binafsi ambacho hakitatozwa kodi kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 50,000/= hadi shilingi 60,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kutoa ufafanuzi kuhusu malalamiko yanayotolewa na watu mbalimbali kwamba Sheria mpya ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 imeongeza sana mzigo wa kodi kwa wafanyakazi.

Aidha, imeelezwa kuwa sheria hiyo inatoza kodi kidogo kwa wafanyabiashara ikilinganishwa na wafanyakazi. Nasisitiza kuwa ili kuondoa utata uliojitokeza baada ya Muswada wa Sheria hii kuchapishwa, Sheria ya Kodi yaMapato ya mwaka 2004 inatumia maneno sawa na yaliyokuwa katika sheria ya zamani ya Kodi ya mwaka 1973 kuhusiana na utozaji wa kodi katika posho mbalimbali za watumishi. Kwa ujumla posho anazolipwa mtumishi kwa lengo la kufidia gharama zinazohusiana na ajira hazitozwi kodi chini ya sheria zote mbili za Kodi ya Mapato yaani ile ya mwaka 1973 na hata hii ya mwaka 2004. Kwa upande mwingine posho za jumla ambazo hazihusiani na gharama za ajira kwa mtumishi zilitozwa kodi chini ya sheria ya zamani na zinatozwa kodi kwa mujibu wa sheria mpya vile vile.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia ya kupanua wigo na kuziba mianya iliyokuwa ikitolewa na waajiri kukwepa kodi iliyokuwa ikitumiwa na waajiri kukwepa kodi, Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 inatoa unafuu mkubwa kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, narudia, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, inatoa unafuu mkubwa kwa wafanyakazi. Chini ya sheria hii, mapato yafuatayo ya wafanyakazi hayatozwi kodi kama nitakavyoeleza:-

(a) Matumizi ya gari la mwajiri, mradi mwajiri hadai unafuu wa kodi kuhusiana na gharama za gari hilo, haitozwi kodi.

(b) Thamani ya nyumba itolewayo na mwajiri ambaye ni Serikali au taasisi inayotegemea bajeti ya Serikali haitozwi kodi.

(c) Huduma ya chakula yaani *cafeteria services* zinazotolewa na mwajiri pale kazini bila ubaguzi katika sehemu ya kazi, hazitozwi kodi.

(d) Gharama za matibabu ya mfanyakazi na familia yake, hazitozwi kodi. *(Makofi)*

(e) Nauli ya likizo kwa mfanyakazi na familia yake, haitozwi kodi.

(f) Sehemu ya mapato ya mfanyakazi inayowekwa kama akiba ya uzeeni katika Mfuko ulioidhinishwa, haitozwi kodi.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hulipia gharama hizi, narudia, wafanyabiashara hulipia gharama hizi baada ya kulipa kodi lakini wafanyakazi husamehewa kodi kutokana na mapato haya. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba wafanyakazi wanaonewa kuliko wafanyabiashara ngazi kwa ngazi katika ngazi hizi za utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile baada ya kutafakari ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, inapendekezwa sasa kwamba mafao ya wastaafu pia yasamehewe kodi. Badala yake kodi hiyo itatozwa kwa Mifuko ya Pensheni ambayo awali ilisamehewa kodi, sasa nairejesha. Lengo la marekebisho haya ni kuwapunguzia wastaafu mzigo wa kodi na kuwawezesha kujijengea msingi mzuri wa maisha ya uzeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya nane, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya vileo ya mwaka 1968 kwa kufuta na kuandika upya vifungu Namba 15 na 16 vya Sheria hii.

Aidha, kifungu Namba 17 kinafutwa. Lengo la marekebisho haya ni kumwezesha mfanyabiashara mwenye leseni ya hoteli au *restaurant* (mgahawa) kuendesha biashara ya vileo ndani ya hoteli au mgahawa huo husika pasipo kuhitaji kuwa na leseni nyingine ya biashara ya vileo ili mradi biashara hiyo ya kileo inaendeshwa na mfanyabiashara huyo huyo mwenye leseni ya biashara ya hoteli au ya restaurant (mgahawa).

Narudia, lengo la marekebisho haya ni kumwezesha mfanyabiashara mwenye leseni ya hoteli au *restaurant* (mgahawa) kuendesha biashara ya vileo ndani ya hoteli yake au mgahawa husika pasio kuhitaji kuwa na leseni nyingine ya biashara ya vileo ili mradi biashara hiyo ya kileo inaendeshwa na mfanyabiashara huyo huyo mwenye leseni hiyo hiyo ya biashara ya hoteli au mgahawa. Nafikiri wafanyabiashara hili wanalielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tisa, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kwa kuweka ufafanuzi wa maneno ili kusisitiza kodi au ushuru ambao Serikali za Mitaa zitakuwa na mamlaka ya kuzitoza kwani imebainika kwamba pamoja na Serikali kufuta kodi za kero zinazotozwa na Serikali za Mitaa Halmashauri nyingine zimeendelea kutoza kodi hizo kwa jeuri.

Aidha, marekebisho mengine yanayokusudiwa ni pamoja na kuweka masharti kwamba ushuru wa mazao utatozwa kodi mara moja tu kwenye Wilaya ambapo zao husika hulimwa badala ya kutozwa ushuru maeneo yote ambayo zao husika hupitia hadi sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile marekebisho mengine yanafuta pendekezo la awali la kuziruhusu baadhi ya Halmashauri kukusanya ushuru kwenye madini ya jasi, pozzorana na chokaa. Pendekezo hilo sasa limeondolewa kama nilivyoeleza wakati wa majumuisho ya hotuba yangu ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Hitimisho la Utumishi wa Umma ya Mwaka 1999, katika kifungu cha 82 ili kuwawezesha wastaafu waliochukua malipo ya pensheni kwa mkupuo zaidi ya miaka kumi iliyopita kurejeshwa katika daftari la wastaafu kwa kuzingatia taratibu za malipo ya pensheni kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na moja, inakusudia kufanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1972. Katika eneo hili inapendekezwa kufuta vifungu Namba 9,10 na 14 vya sheria hiyo vinavyohusu ushuru wa stempu kwenye stakabadhi. Vile vile inapendekezwa kupunguza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye kubadilisha umiliki *(conveyance),* kutoka asilimia nne kwenda asilimia moja ya thamani ya mali husika na kupunguza kiwango cha ushuru wa stempu kwenye kubadili umiliki wa ardhi ya kilimo kuwa shilingi 500/= tu.

Mheshimiwa Spika, lengo la marekebisho haya ni kupunguza gharama za ununuzi na uuzaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na mbili, inakusudia kufanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya mwaka 1997. Katika eneo hili marekebisho yafuatayo yanapendekezwa:-

(a) Kurekebisha jedwali la kwanza ili kutoza kodi kwa kiwango cha sifuri *(zero rate)* kwa bidhaa zifuatazo zinapozalishwa hapa nchini.

(i) Madawa ya kuua wadudu, mbolea, vifaa vya kilimo, madawa na vifaa vya mifugo, nyavu na vifaa vya uvuvi pamoja na injini za mitumbwi ya uvuvi ili kuhamasisha zaidi uzalishaji katika sekta ya kilimo ufugaji na uvuvi. *(Makofi)*

(ii) Madawa, vyandarua na vifaa vitumikavyo kwa walemavu.

(b) Kurekebisha jedwali la pili la sheria hiyo kwa kutoa msamaha wa *VAT* kwa chai inayolimwa hapa nchini na kusindikwa au kuwekwa kwenye vifungashio yaani *locally grown, made, blended or packaged tea* kwa lengo la kuhimili ushindani katika soko la Afrika Mashariki na kulinda mapato ya wakulima wote wa chai nchini. *(Makofi)*

(c) Kurekebisha jedwali la tatu la sheria hii kwa kufuta kifungu Namba 9(1) ili kutoa unafuu wa *VAT* kwa magari yanayoagizwa au kununuliwa na Mashirika ya Dini kwa shughuli za kidini kwa magari yaliyomo chini ya ushuru yaani *tariff heading No. HS Code No. 87.03, 87.02, 20.10* na *No. 8702.90.20* yenye *engine* ya uwezo wa zaidi ya *CC 3000.*

(d) Kurekebisha kifungu Namba 2(A) cha sheria hii ili kuwezesha *capital goods,* mitambo na vifaa na huduma zitolewazo na makandarasi vya miradi inayogharamiwa na Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika sekta ya miundombinu na huduma za maendeleo kama vile maji, umeme na barabara, kupata msamaha wa kodi ya *VAT.* *(Makofi)*

(e) Aidha, katika kupanua wigo wa mauzo ya nje na kuliongezea Taifa mapato ya fedha za kigeni inapendekezwa kujumuisha bidhaa zinazozalishwa humu nchini na kuuzwa katika maduka ya forodha yaani *duty free shops* katika wigo wa *deemed exports* ambapo *exports* haina kodi ya *VAT* kawaida. Hatua hii inalenga kuwafanya wale wenye maduka hayo kuuza pia bidhaa za viwanda vyetu vya hapa nchini kama bia, sigara na kadhalika kwa fedha za kigeni badala ya zile za nje tu ambao ndio utaratibu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa pia kutoa msamaha wa *VAT* kwa huduma za ukaguzi wa mizigo yaani *destination inspection* zinazotolewa na Mamlaka ya Mapato *(TRA)* ili kupunguza gharama kwa waingizaji bidhaa nchini

(f) Kufanya marekebisho katika vifungu Namba 27 na 28 ili kumpa mamlaka Kamishna wa *VAT* kuondoa adhabu na riba au sehemu ya adhabu na riba kwenye malipo ya *VAT* pale ambapo Kamishna ataona ni busara kufanya hivyo mfano baada ya utata kufafanuliwa na maelekezo kutolewa.

(g) Kutoa unafuu wa kodi kwa nyuzi *(yarn)* zinazozalishwa hapa nchini nyuzi za katani, pamba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na tatu, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Elimu ya Ufundi Stadi na Mafunzo ya Mwaka 1994 ili kutoa msamaha wa tozo la mafunzo ya ufundi stadi yaani *Skills Development Levy* kwenye ajira katika mashamba na pia kufanya marekebisho kadhaa katika vifungu mbalimbali ambavyo vimetokana na kutungwa kwa Sheria mpya ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kumi na nne na ya mwisho, inapendekeza kurekebisha Sheria ya Rufani za Kodi ya Mwaka 2000, kama ifuatavyo:-

(a) Kuweka uwiano wa kiwango cha malipo ya kodi kinachopaswa kulipwa na mlipa kodi wakati anawasilisha malalamiko yake ya makadirio ya kodi kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato *(TRA)* kuwa theluthi moja ya makadirio yasiyobishaniwa ili kiwango hicho hicho cha theluthi moja kitumike wakati mlalamikaji anawasilisha malalamiko yake kwa Bodi ya Rufani za Kodi baada ya kutoridhika na uamuzi wa Kamishna wa *TRA.* Chini ya utaratibu wa sasa mlalamikaji anapaswa kulipa nusu ya

kodi iliyokadiriwa ambayo haibishaniwi wakati anawasilisha malalamiko yake mbele ya Bodi ya Rufani za Kodi.

(b) Kuainisha bayana hatua zinazopaswa kufuatwa na mlalamikaji wa kodi ya makadirio kuanzia ngazi ya Kamishna wa *TRA* hadi Bodi ya Rufani za Kodi ikiwa ni pamoja na muda wa kutoa notisi. Sheria ilivyo hivi sasa haikuweka bayana utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ninayopendekeza kimsingi ni ya kiutekelezaji wa mapendekezo ya Serikali ambayo yalikubaliwa na Bunge lako Tukufu wakati wa mjadala wa hotuba ya bajeti. Kama nilivyoeleza hapo awali lengo la marekebisho haya ni kuinua kilimo kwa kuvutia uwekezaji katika sekta hii na papo hapo kuwezesha wakulima wadogo kuongeza tija na kujiondolea umaskini.

Vile vile kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kwa kuwapunguzia gharama za kuanzisha biashara na hivyo kuwawekea mazingira mazuri ya kuwawezesha kufanya biashara halali na kuingia katika sekta rasmi. Aidha, marekebisho haya yanalenga kuinua hali za wastaafu na kuwapunguzia mzigo wa kodi na hatimaye kuwawezesha kujijengea msingi mzuri wa maisha ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ili kuwasaidia wale wanaojiandaa kuchangia hoja hii nikumbushe kwamba Muswada huu kazi yake ni nini. Iko kwenye madhumuni na sababu za Muswada ambazo tulishazigawa muda mrefu, kukumbusha tu kwamba Muswada huu unakusudia kufanya mabadiliko katika sheria mbalimbali za fedha na kodi kwa nia ya kuweka au kubadilisha viwango vya kodi na ushuru.

Kwa hiyo, haihusiani na matumizi ya fedha. Mjadala wa matumizi tulishamaliza, sasa tuko upande wa mapato. Hilo la kwanza.

La pili, marekebisho tumewagawia asubuhi na Mheshimiwa Waziri ametaja kwenye hotuba yake, kwa hiyo, wanaotaka kujadili wakumbuke marekebisho haya ili wayazingatie. Sasa namwita Mwenyekiti au mwakilishi wake.

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA (k.n.y. MHE. NJELU E.M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati baada ya kuchambua na kuujadili Muswada wa Fedha wa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 70(2) cha Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada uliotajwa hapo juu ambao unakusudia kufanya mabadiliko katika sheria mbalimbali za fedha na kodi kwa nia ya kuweka au kubadilisha viwango vya kodi na ushuru.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Muswada huu pia unakusudia kuboresha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu la mwezi Aprili, 2004 hapa Dodoma. Ni matumaini ya Kamati kuwa ili kufanya Sheria ya Kodi ya Mapato iweze kutekelezwa kwa uwazi, usawa na mafanikio zaidi, mabadiliko kama haya ni vema yakaendelea kufanyika pale itakapoonekana inabidi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu uliopita neno kodi limekuwa kama ni kero kwa wafanyabiashara hususan wadogo wadogo ambapo wakati wote kodi hizo zimekuwa zinasababisha mazingira magumu ya kibiashara. Aidha, kutokana na mabadiliko haya ni dhahiri mazingira yanayojengeka yanaashiria vivutio kwa wafanyabiashara kujituma kulipa kodi kwa hiari yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichukua muda wa kutosha wa kujadili vipengele mbalimbali vya Muswada huu na kubaini kuwa bado upo umuhimu wa kuendelea kuziboresha sheria zetu za fedha na kodi ili ziweze kwenda sambamba na mazingira yanayotawala katika maendeleo ya hali ya uchumi. Aidha, sambamba na hilo, kuendelea kuboresha pia sera za fedha na maendeleo ya jamii za ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, majadiliano ya Kamati, yalilenga sana katika maeneo ya kuwepo kwa unafuu wa kodi zinazotozwa kwenye zana na mitambo ya kilimo, madawa ya kilimo, vivutio kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, upanuzi wa wigo wa kukusanya kodi na jinsi ya kupunguza mzigo wa kulipa kodi kwa wafanyakazi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano ya kina, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikubali kuyafanyia kazi kwa mwaka huu wa fedha wa 2004/2005 na pale itakapobidi kwa baadhi yake aweze kufanya marekebisho yanayostahili katika siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo Kamati kimsingi imekubaliana na Mheshimiwa Waziri ni kama ifuatavyo:-

Katika kuisaidia sekta ya kilimo, Serikali ifikirie kuweka viwango vya chini vya kodi za kulipia zana, mitambo na vitendea kazi vinavyoambatana na shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo na hata ikibidi kufuta kabisa kodi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ifikirie pia kupunguza ushuru wa mazao unaotozwa katika vituo mbalimbali vya mauzo kuanzia Vijijini, Wilayani hadi wakati wa kusafirisha nje ya nchi. Pia Serikali iweke utaratibu wa kutoa vivutio kwa asilimia fulani pale malengo ya nje ya nchi yanapovukwa. Wakati Kamati ilipojadili Muswada wa Kodi wa mwaka 2004, mwezi Aprili, 2004, Kamati ilipendekeza kufuta au kuifanyia

marekebisho ibara ya 7(ii) ambayo ilikuwa inakusudia kutoza kodi aina zote za mapato ya mfanyakazi kama vile posho ya kujikimu, posho ya likizo, pango za nyumba na gharama za maisha kwa ujumla. Ibara hiyo imeletwa tena kwenye Muswada wa Fedha wa 2004 na Kamati inaishauri tena Serikali kuiweka ibara hii pasipo kuathiri kipato cha wafanyakazi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya mwaka 2004 imeweka pia kiwango cha *threshold* yaani kiwango cha chini kinachotozwa kodi kwa wafanyakazi kwamba kiwe shilingi 50,000/=. Hata hivyo, Kamati wakati inajadili Muswada wa kodi ilipendekeza kiwango hicho angalau kifikie shilingi 100,000/= na sasa Muswada wa Fedha wa mwaka 2004, umependekeza kiwango hicho na kuwa shilingi 60,000/=. Kamati bado inashauri kiwango hicho kifikiriwe kuongezwa sambamba na hali ya maisha ya wananchi wa kawaida hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoza kodi michango ya akiba ya uzeeni na mafao ya mwisho mtumishi anapostaafu, Kamati imependekeza michango ya kila mwezi na malipo ya mwisho yasamehewe kutozwa kodi lakini mapato yanayotokana na Mifuko ya Pensheni yatozwe kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jitihada za kupanua wigo wa ukusanyaji wa kodi, Kamati inashauri tafiti mbalimbali zifanyike za kuwatambua rasmi walipa kodi wakiwemo wafanyabiashara ndogo ndogo ambao hawalipi kodi ili nao waweze kuingia katika wigo wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kuwa benki zilizopo hapa nchini zimekuwa na ujazi mkubwa wa ukwasi wa takriban wa shilingi bilioni 960 na ambazo kati yake zimewekezwa katika amana na Serikali na haziwekezwi katika sekta nyingine za uchumi, ni vema Serikali ikatoa elimu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo juu ya kupata mikopo kutoka katika benki hizo ili hatimaye wapevuke na kuwa wafanyabiashara wakubwa ambao watalipa kodi kwa uhakika. Kamati inaipongeza benki ya *Standard Chartered* kwa kuendesha semina fupi kwa Kamati hii na ile ya Kilimo na Ardhi juu ya jinsi gani Watanzania wawezeshe kupata mikopo kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika azma hiyo hiyo ya kuongeza ukusanyaji mapato, inashauri elimu ya kutosha itolewe kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na ambao hawaweki kumbukumbu za shughuli zao ili waweze kulipa kodi kwa viwango vya uhakika kuliko ilivyo hivi sasa kodi ambazo hukadiriwa bila kuanishwa kwa kumbukumbu za biashara zao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri vile vile kwamba *natural gas* isitozwe kodi. Waziri aliafiki ushauri huo na pia Kamati ilishauri Serikali irekebishe taratibu za Visa ili kuondoa usumbufu wa wageni wanaokuja nchini kama sehemu ya kivutio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kamati yetu kuwa zoezi la kurekebisha mifumo ya ukusanyaji kodi ni endelevu na ili hatimaye kodi hizo zinazotozwa kwa wananchi zisiweze kuwa mzigo wa maisha magumu kwao. Aidha, Kamati inaipongeza

Serikali kwa kukubali utaratibu wa kutoza kodi za leseni mara moja kwa wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kushiriki kwa ukamilifu katika kuujadili Muswada huu kuanzia tarehe 26 hadi tarehe 27 Julai, 2004 na kukamilisha majadiliano hayo tarehe 2 Agosti, 2004 kwa michango na maoni yao mazuri ambayo kwa kiwango kikubwa yamesaidia sana kuboresha Muswada huu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Lephy Gembe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Idd Simba, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Stanley Kolimba na Mheshimiwa Suleiman Sadiq.

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Hasnain Murji, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Issa Mohamed Salim, Mheshimiwa Rostam Aziz na mimi Mheshimiwa Raphael Chegeni na bila kumsahau Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Katibu wa Kamati, Ndugu James Warburg. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, kumshukuru na kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, Manaibu wake, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa kujibu na kutoa fafanuzi mbalimbali kutokana na hoja za Waheshimiwa Wabunge na hivyo kusaidia Kamati kufanikisha kujadili na kupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha maoni kuhusiana na Muswada wa Fedha wa Mwaka 2004 *(The Finance Act, 2004)*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kutupa nafasi hii ili tutoe maoni yetu ya Kambi kuhusu marekebisho ya Muswada wa Fedha 2004 *(The Finance Act, 2004)* kwa mujibu wa kanuni za Bunge wa kifungu 43(5b) na (c) cha Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa hakuna Serikali yoyote inayoweza kutoa huduma bora kwa watu wake bila watu hao kulipa kodi mbalimbali zinazopangwa na Serikali yao. Lakini ni kweli kwamba sehemu kubwa ya kodi zetu huchangiwa na wafanyakazi wa Taifa letu. Pamoja na kipato kidogo wanachokipata wafanyakazi wetu na hali ngumu ya maisha lakini lazima tukubaliane na ukweli kwamba wafanyakazi hao wamekuwa wahimili wakuu wa mapato ya Serikali na imekuwa rahisi kwa Serikali kukusanya kodi kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi kwa sababu Serikali yenyewe ina uwezo wa kudhibiti mapato ya wafanyakazi kuliko walipa kodi wengine.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunataka kuwapongeza wafanyakazi wote kwa mchango wao mkubwa katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wa pili wa mapato yetu kama tunavyofahamu unatokana na sekta ya uzalishaji na wafanyabiashara. Katika makundi haya mawili ya kulipa kodi kundi pekee lisilo na ujanja wa kukwepa kodi ni hili la wafanyakazi ambalo linakatwa na mwajiri na kuwasilisha kwenye Idara yaKodi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kundi hili la wafanyakazi pamoja na Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa orodha mbalimbali za namna wanavyosamehewa au wanavyopunguziwa makali ya kodi, hakuna hata wakati mmoja Serikali inawaza kuwafutia kabisa kodi au kuwasamehe kodi wafanyakazi maana hata mkondo wao wa kulalamika kawaida haupo rasmi sana kama ulivyo kwa wafanyabiashara. Mara nyingi wanategemea Serikali na kwa kiwango fulani ushawishi wa Wabunge ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kundi la pili la wazalishaji na wafanyabiashara ndilo kundi tunalolitegemea kuchangia kwenye kodi pamoja na kundi hili kwa kiasi fulani kuongeza kulipa kodi, lakini ndilo limekuwa kundi linalopata misamaha ya kodi ya moja kwa moja, lenye uwezo wa kushawishi Serikali kupunguziwa kodi na lenye uwezo wa kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, katika kundi hili kuna lile la wafanyabiashara wadogo wadogo *(Informal Sector).* Kundi hili ni kubwa pamoja na kwamba bado lina uwezo mdogo wa kulipa kodi lakini bahati mbaya bado hakujakuwa na utaratibu wa kukusanya hata hiyo kodi ndogo waliyo na uwezo wa kutoa.

Mheshimiwa Spika, kishawishi kikubwa cha wananchi kulipa kodi ni namna kodi hiyo inavyotumika. Uzoefu umeonyesha pale matunda ya michango yao inapoonekana wachangiaji huwa hawana ubishi wa kuendelea kuchangia. Hivyo hivyo pale walipo wanapoona matunda ya kodi yao huwa hawasiti au kuwa na mashaka ya kuendelea kulipa.

Kambi ya Upinzani inashauri kuwa ili wafanyakazi waweze kuchangia vizuri katika kulipa kodi, Serikali ifikirie namna bora ya kuweza kunyanyua mishahara yao hasa mishahara ya chini ili waweze kuingia kwenye fungu la walipa kodi. *(Makofi)*

Pia wafanyabiashara na wazalishaji ambao sheria mpya inawaruhusu kujikadiria kodi ni vizuri kukawa na uhakiki kwa kutumia uhakiki ambao haukushiriki katika kukadiria yaani *independent body.*

Pia tunashauri kwamba utaratibu wa kukusanya kodi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo ni vizuri ukaandaliwa kwa kufanyiwa utafiti wa kutosha ili kuondokana na usumbufu na pili kukusanya kodi inayostahiki kukusanywa na pia tunashauri kwamba ili kuondoa usumbufu kwa walipa kodi Serikali na hasa Idara ya Kodi ianze kufanyia utafiti utaratibu wa kuwa na Kituo kimoja tu cha kukusanya kodi zote au mapato yote. Utaratibu huu ambao unatumika sana India umesaidia sana kupunguza usumbufu, kuokoa muda ambao ni muhimu katika uzalishaji na kuweza kufuatilia kwa urahisi wale ambao hawajalipa kodi.

Mheshimwia Spika, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali kukusanya kodi kumekuwa na upungufu wa ukusanyaji wa kodi yaani *under collection* mwaka hadi mwaka. Mfano mwaka 2001/2002 kulikuwa na kusanyo pungufu la shilingi bilioni 15, kiwango hiki si kidogo kwa nchi maskini kama yetu. Hivyo, tunaishauri Serikali iongeze bidii katika ukisiaji na ukusanyaji wa kodi ili kupunguza naksi katika bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ya jumla, Kambi ya Upinzani inakubaliana na mapendekezo ya Muswada wa Fedha uliowasilishwa na Waziri wa Fedha. Ila tunapenda kushauri katika Sheria Kuu *Principle Act, section 16* kwamba pamoja na mabadiliko yaliyopendekezwa ya haki ya mkadiriwa wa kodi kulalamika.

Kambi ya Upinzani inashauri kuwa mahusiano kati ya mlipa kodi na mkusanya kodi yazidi kuimarishwa ili Idara ya Kodi isionekane kuwa inatumia nguvu ya ziada pale isipohitajika. Kwa mfano, kufunga biashara ya mfanyabiashara pale ambapo hawakukubaliana kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia tunashauri kwamba kwa kuwa walipaji kodi wetu wengi tunafahamu uelewa wao na kiwango chao cha elimu ni vyema sheria hizi za kodi zikatafsiriwa kwa Kiswahili lugha wanayoitumia na kuielewa kwa umakini. Vinginevyo watakuwa wanaendesha biashara zao bila kufahamu vizuri sheria za kodi zihusuzo biashara wanazozifanya au wanazozitegemea kuzifanya na matokeo yake kuingizwa kwenye makosa ambayo walikuwa hawajaelewa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza Kambi ya Upinzani hatuna pingamizi na Muswada uliowasilishwa kwetu. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOB. Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada ulioko mbele yetu. Lakini nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kipindi chote hiki cha bajeti kwa kutuletea bajeti ya Serikali na kwa kutuletea bajeti ya Wizara yake na sasa hivi kutuletea marekebisho ya sheria mbalimbali za kutekeleza yale yote yaliyoahidiwa katika kipindi chote hiki cha miezi miwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ningependa kuanza kwa kumsifu Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuwa mfanyakazi makini sana lakini kubwa zaidi kuwa msikivu. Nasema ni msikivu kwa sababu hata kama mtu ulisikiliza maoni yaliyotolewa na Kamati, mengi tayari alikwisha yafanyia kazi. Ndiyo maana nasema nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na ile *schedule of amendment* ambayo Mheshimiwa ameileta ukurasa wa 5 kuna *table* pale juu. Ile *table* inahusu kodi inayotakiwa kulipwa kama mtu anatunza kumbukumbu kwenye *column* moja na kodi anayotakiwa kulipa mtu kama hatunzi kumbukumbu. Sasa mtaona *heading* zake pale hazitofautishi anayetunza kumbukumbu ni ipi na asiyetunza kumbukumbu ni ipi. Ni jambo la kurekebisha tu ni *typing error* mahali.

Mheshimiwa Spika, lakini pili katika *table* ile ile kwenye eneo la kwanza la kodi ambapo Mheshimiwa Waziri anasema *where turnover doesn't exceed three million* kodi yake itakuwa shilingi 35,000/=. Pendekezo langu ni kwamba katika eneo hili ukitazama ukurasa wa nyuma wa nne kuna *table* pale ya kodi za nyumba ambayo mfano wake kwa yule atakayekodisha nyumba yake na anapata kipato kisichozidi 720,000/= hatolipa kodi. Sasa hapa ninachopendekeza kwenye hii table ya ukurasa wa 5 tungetafuta *minimum entry point* pia. Kwa sababu kinachoonekana atakayekuwa na milioni moja, atalipa kodi ya shilingi 35,000/= na milioni mbili, atalipa kodi ya shilingi 35,000/= maana milioni tatu imewekwa kama ndiyo kigezo. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, nikienda ukurasa wa 6 wa *Amendment* hii hii Mheshimiwa Waziri amefanya marekebisho kama tulivyokuwa tumezungumza hapa siku za nyuma kwenye sheria mbili muhimu. Huku nyuma amefanyia marekebisho *Business Licensing Act* na akaifuata *Local Government Finance Act* ya mwaka 1982 kuifanyia marekebisho ya *levy* mbalimbali kama alivyoeleza hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini kama alivyosema yeye Mheshimiwa Waziri kwamba mara nyingi Halmashauri zimekuwa zikitoza ushuru bila kujali sana maelekezo ambayo Wizara imekuwa imetoa. Sasa katika ushuru huu wa leseni za biashara utakuta kwamba *Business License Act* ya mwaka 1972 hasa *Amendment* yake ya mwaka 2002 ile ina *schedule* fulani inayoonyesha kila aina ya biashara na *rates* zake na *licenses* zake kwa *categories* za Manispaa, Halmashauri na kadhalika.

Sasa hapa sina hakika kama Mheshimiwa Waziri alikumbuka ku-*delete* hiyo *schedule* ili Maafisa Biashara kule Wilayani wasije wakatumia hiyo kuendeleza kutoza tena leseni za biashara kwa kutumia sheria ya Biashara. Kwa hiyo, nitaomba tu anifafanulie kama hiyo *schedule* nayo iko *deleted* ili makusudio na malengo ya Mheshimiwa Waziri ya kuwawezesha Watanzania hawa kujiwezesha kiuchumi yaweze kukaa sawasawa na hilo ndilo lilikuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niunge mkono juhudi ambazo Serikali imekuwa ikifanya kupitia hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekuwa akitoa hapa leo asubuhi hasa katika masuala ya wastaafu kwa kuondoa na kusamehe kodi katika malipo yao na

katika mafao yao na kadhalika ili kuwafanya wawe na unafuu wa maisha. Lakini yapo maeneo mawili, matatu, ambayo napendekeza kwa siku zijazo nayo ni ya kuyaangalia.

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza la wastaafu ni lile ambalo mmesema mtaanza mwezi Januari, 2005 kushughulika na wale wastaafu waliolipwa kwa mkupuo wale wa miaka kumi iliyopita.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nashauri kwa siku zijazo tuangalie hata wale wengine tuone utaratibu tu tunaweza tukawapishanisha malipo yao, lakini tuone utaratibu wa wastaafu wetu waliolipwa kwa mkupuo kuona namna ambavyo tunaweza tukawaingiza kwenye daftari letu. Kwa sababu kwa kweli wana hali ngumu sana ni kilio cha wastaafu wa nchi nzima. Kwa sasa ni sawa alivyosema Mheshimiwa Waziri najua linahitaji muda napendekeza kwa siku zijazo.

Pili, iko sheria kwa wafanyakazi wanaopunguzwa kazini akiwa na umri wa miaka 50 halipwi kifuta jasho wafanyakazi wa Serikali. Kwa sababu tu ana miaka 50 au zaidi. Walio na umri wa miaka 20, 30 na kadhalika wanalipwa vizuri zaidi kwa kipengele kile kuliko huyu ambaye ametutumikia kwa muda mrefu na tunayempunguza ni sisi Serikali. Halafu tunasema hatumlipi kwa sababu ya *over fifty.* Nilikuwa nashauri kwamba kipengele kama kile tukitazame kwa sababu ana makosa gani huyu. Kosa lake kuwa na *over fifty.*

Mwisho, kuna watumishi ambao wanapunguzwa kazini wako Serikalini au kwenye Mashirika ya Umma wana haki zote, wako kwenye umri wa miaka 50 na kadhalika wanaambiwa hawatapata malipo yako ya uzeeni hadi ufikie umri wa miaka 60 hili nalo linambagua mtu kwa umri wake tu. Sasa sheria za namna hii ambazo zinamtenga mtu kwa sababu ya jambo ambalo yeye *has nothing to do with it,* mimi nafikiri vitu kama hivi viangaliwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nawapongeza Mawaziri wote, Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu Mawaziri wake kwa kutuleta Muswada huu. Ningependa kuzungumzia kuhusu kile kiwango cha *VAT* kilichoongezwa kutoka biashara ya milioni 20 mpaka biashara ya milioni 40. Naipongeza Wizara imeona mbali na hii japokuwa watu wengine wanaona labda Wizara imefanya makosa, lakini kwa kweli Wizara imeangalia *long term benefit* ambayo Serikali itapata. Mapato mengi yatapatikana na vile vile imewahurumia wananchi wake ambao ndiyo walioifanya hii Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kuhusu *visa.* Mimi nimefurahi sana kwamba *single entry* imefanya dola 20, lakini tuangalie sana mipakani na hao tunaowapa *visa* wasije wakaingia nchini wakafanya mambo kama yaliyofanywa ya ulipuaji wa Ubalozi wa Marekani. Tujihadhari sana kutoa *visa* na sisi vilevile tuwaangalie tunaowapa *visa*

kama tunavyoangaliwa sisi tunapopewa *visa* za kwenda nchi za nje. Tunaambiwa mpaka tupige picha bila ya kofia, bila ya mtandio na bila ya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa ushuru katika vifaa vya kilimo na vinginevyo. Mimi naitahadharisha *TRA* kwamba kuna wafanyabiashara wengine watajaribu kutumia mwanya huo *the abuse of facility* kwa kuagizia bidhaa hizi na baadaye kuziuza kwa faida. Watanzania tuna mtindo kwamba tukipewa fursa tunaitumia vibaya. Kwa mfano, mchele umeondolewa kodi na bei ni ile ile inauzwa madukani. Tumekuwa tunawatajirisha zaidi matajiri na tunawafanya maskini wawe maskini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimefurahi ile *Objection to Tax Assessment to the Commissioner.* Hii ni hatua nzuri sana ni sawasawa na kusema kwamba mti unaokupa kivuli usiukate. Ni faida kwa wafanyabiashara, mfanyabiashara akipelekewa kodi kubwa anaweza kwenda kwa *Commissioner* na *power* hizo alizopewa *Commissioner* nimefurahi na nataka aendelee kupewa *power* hizo za kusamehe au kumtoza kodi. Kazi ya Serikali siyo kuwafanya maskini matajiri, lakini kuwafanya wawe wazalishaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu lingine kwa ruhusa yako ningependa kuzungumzia kuhusu *Production of Natural Gas Songo Songo.* Hii ni *production* kwa nini inaondoshwa kabisa ushuru. Mheshimiwa Waziri ningependa anielezea. Ningeshauri ifanywe *exclusivity* kwa mfano *TANESCO* waondoshewe wao kwa sababu ya umeme rahisi kupatikana nchini lakini isiondolewe moja kwa moja. Kuna wengine ndiyo yale niliyosema watakuja kutajirika zaidi.

Mimi sitaki Mheshimiwa Waziri anipende au anichukie, ninachotaka ni kwamba anione kama ni binadamu na aniheshimu au ni Mbunge mwenzake. *Any production to be Taxed Excise Duty is very important.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu leseni. Leseni za biashara zimekuwa bure kwa wenye biashara ndogo ni jambo nzuri. Lakini tunapotoa leseni za biashara tunatakiwa tuangalie nani tunawapa. Leo tunawapa Wachina wanaouza maua, wanaagiza mabegi ambayo wazawa wanaweza kutengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako nitawapa mfano kule Marekani zamani walikuwepo *Red Indians* kabla ya Waingereza kufika Marekani na leo wanasema leo *Red Indians* kwamba zamani walikuja Waingereza walikuwa wana Biblia mikononi mwao sisi tuna ardhi lakini leo wao wametupa sisi Biblia wamechukua ardhi zetu zote, yasije yakatupata hayo.

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa!

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Kwa kutoa leseni ovyo ovyo lazima Wizara ziangalie. Mtu wa nje apewe leseni kwa mfano, aanzishe *Financial Institution*

*and Capital Market, Shipping Business, Insurance, Electricity Power and Energy Supply Business, Processing and Manufacturing of goods and not selling of goods. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimefurahi kuona kwamba *Excise Duty* imewekwa kwa wale wanao-*Supply Satellite Service* za *cable* lakini nimeona ni ndogo. Asilimia 5 ni ndogo kwa sababu *this is a luxury product.* Watozwe japo angalau asilimia 15 siyo asilimia 5. Kwanza kwa sababu wanaonyesha *unsensored Programmes.*

Halafu kwa nini wale wa *Internet Provider* wanaachiwa *that is also the business* wanatoza dola 50 kwa mwezi na wao watozwe. Mimi huwezi kuniona kwenye *Casino* au nacheza *Slot Machine* au kwenye Taarabu napoteza fedha. Mimi na Serikali yangu nataka niisaidie kwa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la wakulima wadogo wadogo ni umaskini na umaskini huo hautaondoshwa mpaka kodi zote ziondolewe zinazowakera wakulima hasa za mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sina zaidi isipokuwa naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza, naomba niombe Mungu anisaidie kwa sababu tangu nimeingia kwenye Bunge hili sijazungumzia habari kama ninayotaka kuizungumza hapa. Kwa hiyo, ni mara yangu ya kwanza kuzungumzia habari ya Idara.

Mheshimiwa Spika, kazi yetu Wabunge ni kushauri na siyo kutafuta malumbano. Hatutaki kulumbana na mtu, hatulumbani na Waziri wala hatulumbani na wafanyakazi wa Idara.

Mheshimiwa Spika, tarehe 29 Julai, 2004 ilitolewa hotuba ya Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, katika hotuba hiyo mimi nilitoa maelezo kuhusu mfanyakazi wa *TRA* aliyefukuzwa kazi kule Mbeya. Mfanyakazi huyo alifukuzwa kwa sababu alitoa msamaha wa kodi kwa mabati yaliyonunuliwa na Kanisa, Mbeya, akaonekana cheo chake ni kidogo kutoa msamaha akafukuzwa kazi. Huyo alikwenda kwenye Baraza la Usuluhishi la Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Mbeya ulitafuta ushahidi mbalimbali ukapatikana kwamba haikuwa mara ya kwanza kwa huyo mtu kutoa msamaha kwa sababu mkubwa wake wa Idara alikuwa mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wakasema adhabu aliyopewa ni kubwa mno asamehewe, arudi kazini ila apewe onyo. Mkubwa wake wa kazi kwenye kikao hicho akasema yeye hawezi kukubali kushindwa na mwanamke. Sasa huyo mwanamke akawa amepata ushindi wa Baraza la Usuluhishi la Mkoa Mbeya. *TRA* hawakuridhika kwa kushindwa na mwanamke, wakaomba rufaa kwa Waziri. Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, akakaa nadhani Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo inajua

sheria za kazi, wakatoa uamuzi kwamba kwanza tuhuma walizomtuhumu hazikuthibitika. Kwa hiyo, arudishwe kazini. Mtu huyo hakurudishwa kazini.

Mimi nimekuwa nawasiliana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na watu wa *TRA* hata tumezungumza hapa Bungeni na *Commissioner* Mkuu wa *TRA* akaniambia atalipeleka kwenye Bodi na kwamba ana kesi za namna hiyo saba za watu waliopitishwa na Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo kurudishwa kazini, lakini hawajarudi kazini. Mimi nikaona ahaa, basi niache na nikamweleza wazi kwamba mimi na Mheshimiwa Basil Mramba tumefanya kazi *SIDO* kwa muda wa miaka 10 wala sina haja ya kukabiliana naye Mheshimiwa Basil Mramba, ni mkubwa wangu tumefanya naye kazi vizuri sana. Sasa nikaona hakuna kinachoendelea na ndiyo nikasema kwenye hotuba ya Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, athibitishe kwamba alimwona na hatia huyo au hapana. Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo kwa kujibu hoja yangu Bungeni, *Hansard* imetoka ya tarehe 29 Julai, 2004. Mheshimiwa Waziri anasema: "Mheshimiwa Stephen Kahumbi, alizungumzia kuhusu mtumishi wa *TRA,* nataka nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kulifanyia kazi hilo tatizo la huyo mfanyakazi kwa sababu mimi naamini Serikali ni moja na Waziri wa Kazi anapoamua anaamua kwa niaba ya Serikali ile ile."

Kwa hiyo, nadhani Mawaziri wengine vile vile wanajua kwamba lazima tuheshimiane. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo anasema na akakazia kwamba, atarudi kazini ikilazimika atakaza hukumu, imeandikwa kwenye *Hansard* ya tarehe 29 Julai, 2004.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza watu wa *TRA* wanaona kama mimi nina-*confrontation* nao. Leo wameniletea barua kwa *EMS* ambayo haina ukweli wowote. Ninasikitika ninayo hapa yaani baada ya kusikia tunazungumza humu Bungeni wakakaa kule Dar es Salaam kupinga Bunge. Imeandikwa tarehe 2 Agosti, 2004 mimi nilizungumza tarehe 29 Julai, 2004. "Hii ni kukujulisha kuwa msimamo wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania ni kuwa haikubaliani na maamuzi yaliyotolewa na Baraza la Usuluhishi Mbeya kupitia karatasi namba 5 yenye kumbukumbu namba hiyo ya tarehe 12 Desemba, 2001. Mamlaka ya Mapato ilipokea uamuzi uliotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kupitia karatasi namba 8 yenye kumbukumbu namba hiyo ya tarehe 17 Desemba, 2002." Hasemi sasa wanaifanyaje hiyo barua ya Mheshimiwa Waziri. Lakini anaruka anasema: "Tunapenda ufahamu kuwa Sheria iliyotumika katika kulishughulikia suala lako ni Sheria ya Usalama ya Kazini namba 62 ya mwaka 1964 kama ilivyorekebishwa na kitendo namba 1/195 inamruhusu mwajiri kukurudisha kazini au kutokurudisha kazini."

Sheria hii inamruhusu *private employer* siyo *employer* wa Serikali. Huyu mtumishi hakuwa mtumishi wa *Commissioner,* alikuwa ni mtumishi wa Serikali. Mwajiri binafsi anaruhusiwa kwamba mimi unaniambia huyu mtumishi wangu hana kosa, nakubali hana kosa, lakini simtaki. Kwa hiyo, nampa mshahara wa miezi mitatu, *off.* Huyo mtumishi hakuwa mtumishi wa mtu alikuwa ni mtumishi wa Serikali kama *Commissioner* mwenyewe. Kuna *provision* yake na *provision* yake imehukumiwa na

Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo, anadharauliwa *Commissioner* wa Kazi maana yake nini? Tuna Serikali ngapi hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa madhumuni ya kuomba niseme hapa, nilitaka kusema mambo mawili, matatu. La kwanza, mimi sina chuki na watu wa *TRA* wala huyo mtumishi wao, mimi Mbeya sijafika. Sina chuki nao lakini si mwoga kutetea haki ya mtu. Kuna Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameniambia Stephen Kahumbi, acha tu kwani nani, mimi huwa nimezoea kufanya *confrontation* ikilazimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi ukaacha mtu anaonewa kwa kuvunja sheria. Kwa sababu mtu hajui sheria kwamba hii inayosemwa ni ya nani? Kuna sheria mbili, mfanyakazi wa Serikali huwezi ukamhukumu kwa sheria ya wafanyakazi wa ofisi za watu binafsi, kama unamchukia ondoka wewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nikiwa mfanyakazi niliomba uhamisho kutoka shule fulani kwenda shule fulani kupitia kwa *DC. DC* akaniambia wewe unaomba uhamisho kwa kumkimbia *Headmaster,* je, ukipelekwa Sumbawanga naye kesho akahamishwa kwenda Sumbawanga utamkimbia tena? Kaa naye mpambane naye hapa hapa tukapambana mpaka tukaachanishwa yeye kaenda Tabora na mimi nikaenda Sumbawanga. Sasa huu uamuzi wa chuki binafsi, hii ni chuki au ubaguzi, ukabila, mwanamke. Ni kosa kuwa mwanamke? *(Makofi)*

Naomba hilo wafahamu kwamba mimi sina chuki nao. Hawa watu wa *TRA* kama walikuwa wanataka kumfukuza kazi wangempelekea Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo. Hawakumpelekea Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo barua hii aliyesema atakaza hukumu siyo mimi. Sasa kwa nini hawakumpelekea Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo wananiletea mimi, mimi ni nani, mimi ni Mbunge nilikuwa nawashauri tu. Sasa naomba ieleweke kwamba Waziri wa Fedha hawa watu wake kama anawaunga mkono waungane mkono. Ila mimi nakuomba kwa suala hili uitume Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ichunguze ukweli wa hili jambo. Hatuwezi kuvumilia watu wanaonewa kwa sababu ya ubaguzi sijui ukabila au nini haiwezekani. *(Makofi)*

Mimi nimekaa hapa Bungeni tangu mwaka 1985 mlishanisikia nikisema habari ya mtu hapa hata siku moja lakini *they are knowing.* Naomba aidha, Waziri wa Fedha amuunge mkono Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Michezo kwamba huyo mtumishi anarudishwa kazini au basi kwa sababu ni Bunge limedharauliwa na mimi sikusema nje huko kwenye Kantini nilisema hapa hapa Bungeni. Kwa nini kuruhusu Bunge lidharauliwe kiasi hiki? Nilikuwa naomba wakati Waziri wa Fedha rafiki yangu Mheshimiwa Basil Mramba ana-*wind up* anieleza anamwambia huyo amrudisha kazini. Maana Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, aliyesema, sisemi Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya kwa sababu anatoka Tabora. Nilisema hapa Bungeni kwamba ni halali na ni vizuri zaidi, kuchinja kuku wako utalaumiwa na mimi nikasema nakuchinja wewe Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa sababu Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, unatoka Tabora kwa hiyo, nikikutolea shilingi wewe ndiyo vizuri. *(Makofi)*

Sasa na hapa simtetei Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, kwa sababu anatoka Tabora naitetea Serikali, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, ni Waziri wa Serikali, anachosema ni amri watu wa *TRA* lazima wafahamu.Waziri yeyote anaposema ni amri siyo anakubembeleza tutakuwa na Serikali ngapi. Naomba nielezwe kwamba huyo mtu atarudishwa kazini aidha *Commissioner* anampenda au hampendi mimi sijui. Kama sivyo hivyo nina heshima sana nakuomba uitume Kamati ya Fedha na Uchumi, ichunguze ukweli wa kufukuzwa kazi kwa huyo mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu kwa kunipa mara mbili kwa siku moja nafasi ya kuongea kwa kweli nina haki ya kujisifu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru pia hoja aliyoileta Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kweli ni hoja muhimu na ina vipengele ambavyo vinagusa jamii ya watanzania. Lakini tu ningeomba nichangie mambo sita. Jambo la kwanza, ni katika *Community* ya *East Africa* kuna bidhaa 80 zilizotajwa ambazo Tanzania ingeweza kuuza kwa wenzetu wa Uganda na Kenya bila kutozwa ushuru. Lakini katika zile bidhaa sijaona bidhaa za usafirishaji. Kwa mfano, hatukutaja kama tutaweza kutengeneza baiskeli, pikipiki au magari. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri aainishe hili suala kwamba kuna haja pia ya kuona mbele kwa maana kwamba tunaweza pia tukatengeneza vitu kama hivyo.

Kwa hiyo, ningeomba aliweke hili suala liitakuwa na manufaa makubwa sana kwamba mtu ku-*import* gari kutoka Japan itakuwa ni gharama kubwa kuliko kununua hapa, kwa maana hiyo tunaweza kujikuta Watanzania tunapata soko nzuri kama tutatengeneza baiskeli, pikipiki au magari tukayaunda hapa hapa na tukayapeleka kule kwa wenzetu. Zitakuwa na manufaa makubwa sana kwamba mtu ku-*import* gari kutoka Japan itakuwa ni gharama kubwa kuliko kununua hapa. Kwa maana tunaweza kujikuta Watanzania tunapata soko zuri kama tutatengeneza baiskeli, pikipiki au magari, tuyaunde hapa hapa tukayapeleka kule kwa wenzetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninaona uko *busy* na karatasi ninaomba ulisikie hili.

**SPIKA:** Waziri atasoma *Hansard* baadaye.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Kwa hiyo, ninakwenda la pili, ni kuhusu wafanyakazi. Ametaja wafanyakazi kwamba, wanaondolewa kodi, lakini pia wafanyakazi wa aina nyingine kama Waheshimiwa Madiwani, upande wa Halmashauri za Wilaya tunao Madiwani ambao hawapati mishahara moja kwa moja kutoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, tunaposema kwamba wana unafuu wa kodi, bado kuna wengine ambao unafuu huu sio moja kwa moja. Ningeomba hili kuna Waheshimiwa Madiwani, ambao kwa kweli wanafanya kazi kubwa mishahara yao ni midogo sana, hawana nyenzo na wameniomba nifikishe hili wazo kwamba, wanahitaji usafiri. Wao hawana punguzo

lolote kama walivyo wafanyakazi wengine wa Serikali wakiwemo Walimu. Lakini ukiangalia katika Kata zao ndio watendaji wakuu na wanawajibika kwa kila kona kuanzia elimu, afya na kwingine. Sasa wanaomba waondolewe kodi hizi katika usafiri angalau waanze kununua pikipiki ambazo zitakuwa zimeondolewa kodi katika awamu hii ya bajeti kama itawezekana. Kwa hiyo, ninaomba waangaliwe Madiwani waondolewe kodi za *VAT* na ikiwezekana pia *import duty* ili wapate usafiri.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu pensheni. Tumeongelea sana kuhusu pensheni kwamba, zimeboreka. Nitamwomba pia akumbuke kwamba, katika swali langu la wiki iliyopita niliomba wakulima, kwa hiyo, naomba atakapokuwa anajumuisha suala la pensheni pia aangalie wakulima na wafanyiwe kazi katika hilo suala la pensheni.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu boti. Tumeondoa ushuru katika boti za wavuvi lakini hajataja, boti ikija ikaundiwa hapa ikaja *engine* halafu ikatengenezwa boti je, utaratibu utakuwaje? Halafu lingine ni kuhusu ufundi stadi. Tunaondoa kodi lakini pia kuna *machinery and tools*. Hizi ni nyenzo mama kwa maana kwamba, ni sawa na malighafi, ni nyenzo za kutengenezea vifaa, kwa maana hiyo, tunaweza kuita ni malighafi. Kwa hiyo, ninaomba pia aainishe kwamba tunapoondoa ufundi stadi wana *machinery* ambazo zinatakiwa zitumike, je, tumeziondolea *PM?*

La sita ni kuhusu kilimo, tuliondoa kodi za kufyeka. Kwa kweli mimi haiingii kichwani ninapooambiwa kwamba tunaondoa kodi za kufyeka shamba. Kufyeka na sijui mkulima mdogo ataanzaje kuomba punguzo la kodi ya kufyeka shamba. Kwa hiyo, ni kiinimacho hapo. Mimi nikadhani tungekuwa wazi kama kuna watu wanaoomba wanataka aidha Makaburu au watu gani wanataka kuwekeza ambao wanataka waondolewe kodi. Sasa huyu mtu anayekuja kuwekeza tayari ana fedha kama anatoka huko Zimbabwe anakimbia anakuja na fedha zake kwa nini tena tumwondolee kodi ya kufyeka shamba. Kwa sababu sidhani kuna mkulima anataka kwenda kufyeka shamba aondolewe kodi, sidhani. Kwa hiyo, mimi hilo bado linanikunisha kichwa, ni nani tunamwondolea kodi ya kufyeka shamba. Ni mkulima huyu huyu wa eka moja au wanaitwa mabwanyenye wanaokuja. Kama wanakuja wana fedha ni kwa nini tuondoe tena kodi ya kufyeka. Mimi nadhani badala ya kuondoa kodi ya kufyeka tungepeleka kwenye pembejeo. Kufyeka hakuna Mtanzania ambaye ana shamba atakalokuja kuomba msamaha wa kufyeka, sidhani. Kwa hiyo, naomba muwe wazi kwamba, kama kuna watu wameomba tufanye hili na hili au tufanye hiki basi kaondoeni kodi ili hawa jamaa waje.

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho ningeomba pia nimuunge mkono Mheshimiwa Stephen Kahumbi kwamba, ni lazima tutofautishe *political cloud* halafu na *money cloud.* Kwa kweli wafanyakazi wengi wanajisahau sana. Hawajui kwamba hili Bunge ndio mama wa nchi. Ni mama sijui niseme baba, yaani ndiyo mama wa nchi kwa maana kwamba, ndiyo inapanga mambo yote. Fedha zote zinazokwenda *TRA* ndio Bunge linapitisha. Sasa kuna watu wanajisahau, wanasahau kwamba, kuna kitu kinaitwa *political cloud,* kwa maana nguvu ya siasa. Nguvu ya siasa huna fedha lakini una nguvu ya siasa kama Mbunge.

Sasa wengine wakishapata vihela kidogo tu wanasahau kabisa hata ukienda anakudharau, nilikwenda Ofisi moja nikakaribishwa nikaambiwa *actually* nilikuwa na Mheshimiwa Mbunge mwingine nisingependa kumtaja, akatukaribisha akatuambia karibuni mketi. Yaani kiasi kwamba, japo tulikuwa tumekwenda na hoja za Wananchi lakini mtu anaji-*feel* ile *money cloud.* Unajua ni vihela tu akipata shilingi milioni kumi au ishirini anajiona yuko juu. Lakini bado mwanasiasa Mbunge yuko juu tu. Hatuna fedha lakini tuko juu. Kwa hiyo, ningeomba *TRA* mlijue hilo kwamba, hata mkipata chochote mfukoni mwenu bado hawa Waheshimiwa Wabunge wako juu yenu na wakipanga mambo yao msiwaone kama wanapanga vitu ambavyo ninyi hamjisikii kuvifanya. Ni lazima mfanye kama vimepitishwa na Bunge hili na yeyote juu ya Bunge kwa maana kwamba Bunge ndio juu ya wote, Serikali iko chini ya Bunge, Bunge likiamua halina ujanja.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaongea hayo na la mwisho kabisa kwa sababu muda wangu unaniruhusu, ningeomba niongelee masuala ya leseni. Kwa kweli leseni imetupa utata. Watu wengi sana wanakuja kwetu kuuliza kuhusu leseni. Wanauliza kweli zimeondolewa. Akienda kule anaambiwa hii bado haijaamuliwa. Kwa hiyo, ni kwamba, hata wafanyakazi wenyewe wa *TRA* na watoaji wa leseni bado hawajapewa ni nini wafanye. Kwa hiyo, tungeomba utumie nafasi hii ili wapewe shule ya kuhusiana na haya mambo ambayo Mheshimiwa Waziri uliyapendekeza na tukayaondolea kodi. Kwa hiyo, naomba uwape hii elimu mapema iwezekanavyo ili wasitupe utata kule na hivyo wakulima na watu vijana ambao wanataka kupata leseni wakajikuta wanashindwa.

La mwisho kabisa ni kuhusu kodi ya kilimo, kuhusu misitu na mazao. Tumeongea usindikaji lakini kuna vitu vinaitwa *packaging.* Kwa hiyo, pia ninaomba ubainishe kwamba, unapoongelea usindikaji kuna mikopo, magunia, tumeyaweka fungu lipi?

Mheshimiwa Spika, ninaomba nikushukuru kwa nafasi hii na ninaomba kusema tuko pamoja na Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijaanza kuujadili Muswada huu, naomba nichukue nafasi hii, kwa vile ni mara yangu ya kwanza kujihusisha na mjadala kutoka Bunge toka tufiwe na Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kaspira.

Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wananchi wa Mbulu, naomba kutoa mkono wa rambirambi kwa familia na Wananchi wa Ulanga Mashariki, kwa kufiwa na Mbunge wao. Binafsi napata masikitiko makubwa kwa sababu Marehemu alikuwa jirani yangu hapa Bungeni, alikuwa rafiki yangu na tulikuwa tukishauriana mara kwa mara kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Bunge lako na nchi kwa ujumla. Nasikitika zaidi kwa sababu Mbunge aliyemtangulia Marehemu Mheshimiwa Guntram Itatiro, naye tulikuwa tunakaa hapa. Kama mila ingeliruhusu Bunge lako hili lingefanya tambiko katika kiti hiki kwa sababu muda wote mimi nakuwa napata tabu sana nikiwakumbuka wote wawili. Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika na mimi nianze kwa kuungana na Mheshimwa Muttamwega Mgawya, lakini kwa kusema kwamba, si vyema kwa watumishi wa Serikali au kwa raia mwingine yeyote kuulizia matamshi yaliyotoka Bungeni. Kwa sababu yana kinga ya kisheria na ni mbaya sana hasa kama maulizo au dukuduku ya maandishi yanatoka kwa watumishi wa umma. Nasema hivyo kwa sababu wana mwakilishi wao hapa. Waziri ndiyo angeyasema yale ambayo ameandikiwa Mheshimiwa Stephen Kahumbi. Mimi ningesema kwamba, pengine lile lingetolewa kama onyo la mwisho kwamba, si vyema na ni kukiuka sheria ya maadili na haki za Bunge kumwandikia Mbunge kuhusiana na yale aliyoyatamka Bungeni. Niwakumbushe pia kutokufahamu sheria sio kinga. Nisingependa kutamka kwamba, suala hili lipelekwe kwenye Kamati ya Maadili ya Bunge lakini wakati umefika kwa watumishi wa Serikali kufahamu kwamba, wana wawakilishi wao hapa. Hivi viti vyote vilivyoko mbele hapa ni wawakilishi wao, hawana haja ya kuwaandikia Wabunge kuhusu matamshi yaliyotamkwa hapa Bungeni kama ilivyotokea kwa Mheshimiwa Stephen Kahumbi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada ulio mbele yetu, mimi sina mengi sana. Kwa mara ya kwanza, Muswada mfupi sana pengine toka mwaka 1973, kwa sababu Sheria ya Kodi ya Mapato ndiyo tumeipitisha juzi na ndiyo ilikuwa ikifanyiwa kazi na Muswada wa Fedha. Kwa hiyo, mimi nitaongelea kwa kifupi sana na kwanza kuhusu Sheria ya Leseni ya Biashara. Sote tunashukuru kwamba, tumeondoa leseni sasa kabla hata mtu hajaanza biashara. Lakini tatizo lililojitokeza katika kutekeleza azma hii nzuri ni kwamba, kwa mara nyingine tumeendelea kuiondolea Serikali za Mitaa, Halmashauri zetu, kianzio cha fedha. Wiki iliyopita mimi nilihudhuria Kamati ya Fedha ya Mipango na Uongozi ya Halmashauri yangu, kutokana na uamuzi huu, Halmashauri ile imepoteza karibu shilingi 40,000,000/=. Hii sio Halmashauri kubwa, kwa Halmashauri kubwa kama Ilala pengine ni shilingi bilioni moja. Sio chini ya shilingi 500,000,000/=, kwa Halmashauri kubwa ambazo zilikuwa zinategemea leseni.

Jana Waziri wa Serikali za Mitaa, alitoa jibu ambalo halikuturidhisha sana kuhusu hali halisi ya Halmashauri ya Kondoa na Halmashauri nyingine ambazo hazipati fidia kama ilivyokuwa inatarajiwa baada ya kodi za kero kuondolewa. Sasa huu ni mzigo mwingine kwa Halmashauri. Sasa sijui tunakwenda wapi. Tunaweza tukawapendezesha raia kwa kuwaondolea kodi nyingi lakini maana yake pia tunapunguza huduma. Baya zaidi tunaingilia sana Serikali za Mitaa, ambazo kuwepo kwake ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Huu ni mgongano ambao toka mwaka 2003 tumeuona katika eneo la fedha na mimi naona hakuna namna nyingine ya kutatua ni kuwafidia kama ambavyo inatakiwa. Kama Kondoa au Rombo ilikuwa wanakusanya shilingi 300,000,000/= kwa mwaka, fidia iwe shilingi 300,000,000/=. Sasa maombi yataongezeka kutokana na leseni kuondolewa. Mimi naamini Halmashauri kama Ilala, Kinondoni ama Temeke, kutokana na sheria hii ya sasa tutakuwa tumewapunguzia kwa mwaka kati ya shilingi 500,000,000/= mpaka shilingi bilioni moja kwa mwaka. Hii sio haba, naomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie sio tu kwamba tumepunguza uwezo wa kifedha wa Halmashauri lakini ni kuingilia Halmashauri kwa wazi ukimpunguzia mtu nguvu ya kifedha unampunguzia nguvu ya uamuzi. Tunaipunguzia Serikali ya Mitaa uwezo wa kuamua mambo yao, uwezo ambao

unatokana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nisingependa kuliendeleza hili kwa sababu liko wazi.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nilisemee ni Sheria ya Pensheni. Napenda kuanzia hili sijui kama limesemwa, kama limesemwa naomba utanisamehe nalirudia. Hivi kuna nini kinaendelea sasa katika malipo ya pensheni? Waziri angekwenda hapa Dodoma hamna aliyelipwa fedha mpaka leo. Leo ni tarehe 5 Agosti, 2004, Dar es Salaam pia nasikia hawajalipwa. Asubuhi nimeongea na Wilaya yangu hawajalipwa, kuna nini kimetokea? Ni unyanyasaji tu wa wazee au nini? Hili mimi ningeomba Waziri leo atoe tamko rasmi, kwa sababu hao watu wametoka mbali Vijijini. Mimi Jumamosi *(weekend)* yote iliyopita nilikuwa nyumbani, walishaanza kufika Mjini wakitarajia Jumatatu tarehe 2 Agosti, wangeanza kupokea pensheni. Sasa hao watu huhangaika sana Mjini. Ili wazee wetu na ni haki yao kwanza ni miezi saba imepita hawajalipwa, tunaambiwa utaratibu umebadilishwa.

Kwa nini tangazo lisitolewe tena miezi hii sita au saba iliyopita? Dar es Salaam nasikia wanaambiwa kwamba, itabidi waende sijui Jengo la *NSSF* pale karibu na Stesheni ya Reli, Benki haitaweza kulipa. Nilipoongea na Ofisa wa Hazina wa Wilaya yangu, waliniambia kwamba, pengine ni majina tu yatafikishwa Benki na viwango havijulikani ni kiasi gani. Usumbufu huu ni wa nini, hebu Waziri atueleze na atume mtu wake sasa hivi hapa Dodoma kwamba, hapa Dodoma sio mbali sana ni mwendo wa dakika tano. Kwa nini wastaafu hawalipwi wiki hii? Wengi wametoka mbali Vijijini, naona wanasongamana hapa Mjini, matatizo makubwa, hawana wa kumtegemea, hebu tuelezwe.

Sasa kuhusu wale ambao walipokea pensheni kwa mkupuo, sisi wote tumetoka Vijijini kama wako waliokulia Mjini ni wachache. Vijijini nyumba zetu sio nzuri sana, kuna mende, panya, makaratasi yanaliwa. Sasa hawa wazee wengi inawezekana wamepoteza makaratasi. Wamepoteza nyaraka mbalimbali lakini wako hai. Wana haki ya kurejeshwa kwenye orodha ya kulipwa pensheni. Ningeomba Waziri akubali ushauri wangu wa kwamba, waape mbele ya Hakimu wa Mahakama wa Mwanzo, Mwanasheria aliye karibu waape *affidavit* kwamba, bado wapo hai. Iwapo kuna nyaraka chache zinazoonyesha kuwa aliwahi kuwa mtumishi na aliwahi kulipwa kwa mkupuo. Kwa sababu kama tutafuata sheria kama mashine kwa kweli hawa wazee hawatarejeshwa kwenye rejista kwa sababu kupata *document* zote na kama tunavyoelewa maisha yao hawa kule Vijijini yalivyo sio rahisi.

Mheshimiwa Spika, kuna maelezo kwamba, kutoka kwenye orodha ya pensheni itaongeza hawa ambao wamelipwa kwa mkupuo. Mimi uelewa wangu ni kwamba, kwa sababu wale ambao hawakulipwa kwa mkupuo walikuwa wakipata nyongeza na sio nyongeza ndogo nyongeza kubwa. Ndiyo maana hawa ambao waliochukua mkupuo wameshawishika kwamba, mbona mambo sasa ni mazuri. Bila shaka Waziri tofauti hii ataiwekea maanani hapo Januari atakapowalipa wastaafu hawa kama amenielewa vizuri. Kwamba, tofauti kati ya kiwango walicholipwa wakati wamechukua kwa mkupuo na kiwango cha leo nafikiri itakuwa ni haki yao na Serikali wahusika wajitahidi ku-*compute.* Sio kwamba sasa tunaanza kuwalipa upya. Kwa sababu ukichukua kwa mkupuo haikuwa

ni kosa lao, ni Serikali iliwapa *option* na wao wanarejea leo wakitarajia kwamba, manufaa waliopata wenzao walibaki kwenye orodha ni manufaa hayo watayafaidi. Mimi nafikiri hilo sio tatizo kubwa sana la kisheria. *Actually* tunatekeleza haki na tunadai kisheria zaidi kuliko vinginevyo, kama Waziri atakuwa amenielewa naomba basi atuambie wazi wazi kwamba, hawa watapewa tofauti hii ambayo wenzao waliobaki kwenye orodha walikuwa wakipata hasa kuanzia mwaka 1995 hadi leo baada ya Serikali ya awamu ya tatu kuingia madarakani na kuboresha mafao ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na mimi pia naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Muswada huu muhimu wa *Finance Bill.*

Kwanza, lazima nitoe shukrani zangu na kumpongeza sana Waziri na Manaibu wake, kwa juhudi kubwa wanazozifanya kuhusiana na masuala ya fedha na hasa hali yote kwa ujumla kuhusiana na namna tunavyokusanya mapato sasa na kuendesha nchi yetu. Mimi ningependa tufike mahali sasa tuweze kabisa kujitegemea au twende zaidi ya kiwango tulichofikia sasa cha mapato yetu sisi wenyewe.

Labda tu nina machache kwa sababu mengi naona yameshazungumzwa na tunazungumzia kitu kimoja hiki. Ningependa tu nianzie na hoja kwamba, mengi katika hii *Finance Bill* tuliangalia na kuyakubali wakati tukipitisha bajeti yetu ya mwaka 2004/2005. Hii ilisubiri tu kwa ajili ya kuleta utekelezaji na kumpa Waziri nguvu zaidi aweze kusimamia bajeti yetu hii ya 2004/2005. Taratibu tu ni kwamba, labda hii ilipaswa sijui ingetangulia au sijui ingekuja pamoja na bajeti yenyewe, ili twende pamoja na jambo zima hili badala ya kulibakiza nyuma. Lakini kwa sasa limefafanua mambo mengi na nina imani kwamba, litafanya sasa hali iwe sawa sawa na watu waweze kutekeleza majukumu yao hasa watendaji ambao wanakuwa wazito kutekeleza maagizo haya wakati yakitolewa na Serikali katika majadiliano ya kupitisha bajeti yetu ya mwaka 2004/2005. Kwa mfano, ukisoma hii *Finance Bill* inasema kwamba, mengi yote yatahusika na yanahusika kuanzia tarehe 1 Julai, 2004 na kama yameanza kuchelewa kutekelezwa basi ni kutofuata tu na kutokusikiliza maagizo ya Serikali yanakwenda namna gani.

Mimi nina mawili ningependa niyasemee kuhusiana na *Income Tax, schedule* ya tano hapa ambayo imeelekezwa. Nikizungumzia na kujielekeza kwenye kodi ya pango. Kwenye kupanga imeonekana kwamba, kuna kiwango ambacho kinatolewa ambacho mtu halipi kodi kutoka pale kama kinazidi basi analipa asilimia 15 ya mapato ya pango hilo. Kikubwa tu ambacho nataka kuelezea ningeshauri labda hii sehemu ya chini ya *allowance* ambayo anaruhusiwa mtu kukaa nayo bila kutozwa kodi, ingepandishwa kidogo. Kwa sababu kwa kweli *property* inakuwa na kodi nyingi sana. Kuna kodi ya kiwanja, kodi ya *income tax* lazima ulipe, kuna *house levy* kama tatu, nne hivi, jambo ambalo linakuwa ni *too much* kwenye sehemu moja hiyo ya kutozwa kodi. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri aangalie hilo kama linawezekana alipatie nafasi ili kwamba wanaokuwa na *properties* basi nao wafaidike kidogo, wasizungukwe na mlolongo wa kodi nyingi kama hizo ambazo zimeelekezwa na zinataka zote zitozwe bila kujali ni nini

ambacho huyu mtu abakize na kuwatia moyo watu waweze kuwa na *properties,* wasiwe waoga kujenga na kuandaa *properties* kwa ajili ya matumizi ya jamii yote.

Mheshimiwa Spika, kingine nilitaka kuelezea tu na kufafanua kidogo suala zima la nani apewe leseni zipi. Tuna wageni, nakubali na sisi wenyeji ni wenyeji. Sasa tunapowekwa wote sawa kwa kweli mimi hapo tu ndio najaribu kukwama. Kwa sababu kama tumetoa kiwango kwamba leseni inapotolewa ada isitozwe mpaka biashara izidi shilingi 20,000,000/= na sasa hivi kuna wageni wanafanya biashara nyingi zilizo chini ya shilingi 20,000,000/=. Sasa hao nao watapewa leseni jumla kwa hali moja kwa moja na sisi. Pamoja na hilo pia kuna hali hii nzima ya kodi zingine ambazo zimesamahewa kwa mfano kodi ambayo imetolewa wakati mtu ukiandaa shamba. Sasa ni nani apewe kodi hii, apate msamaha huu. Kwa kweli mimi ningependa tu Waziri awe kidogo makini zaidi ili kwamba itakapofaidika basi tufaidike sio kuwafaidisha kila mtu, suala hili mimi kwa kweli bado halijanikaa vizuri. Ningependa afafanue zaidi na aelekeze hii hasa maagizo haya yamguse nani kwa sababu raia lazima apewe nafasi yake kama raia na wengine waingie kama wageni wakijijua kwamba, wana nafasi au kama wageni ili twende nao sawa wasije watatutawala kabisa wakatunyang'anya mali tukashindwa la kufanya.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningependa niseme ni kwamba, nashukuru sana juhudi ambazo Wizara na Serikali inaziangalia. Suala zima la kuondoa umaskini, suala zima la kumpunguzia mkulima mlolongo wa kodi. Katika agizo hili kwenye sehemu ya *Local Government Act No. 9* kuhusiana na utaratibu wa kutoza kodi za mazao mara mbili, hii kwa kweli imemsaidia sana mkulima na Wananchi kwa jumla ambao wanasimamia kazi hizi. Kwa hiyo, mimi ningependa tu kusema kwamba, jambo hili lingesisitizwa likaziwe na lieleweke lisije likarudiwarudiwa kutolewa ufafanuzi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninapenda tu nikazie sana suala la pensheni. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Marmo. Mimi sikubali kwamba, Vijijini peke yake wana tatizo hili. Mimi ni Mbunge wa Mwanza Mjini, niko Mjini pale, malalamiko ya watu kuhusiana na pensheni ni makubwa sana. Hali iko wazi kabisa ikifanana sawa na watu wa Vijijini. Mimi naona tu labda ni tatizo la utendaji. Watendaji wanakuwa wazito au hawataki sijui kuwapa hawa watu pensheni, mimi sielewi. Lakini ukweli ni kwamba, usumbufu huu na majukumu ya Wizara kama Wizara labda ningeiomba Wizara iboreshe hiyo Idara inayohusiana na ulipaji wa pensheni, usimamiaji wa pensheni kwa Wananchi wetu hawa ili kwamba kazi hii ifanyike kwa ufanisi wa juu zaidi.

Mimi naona kama sijui wanawahesabu wameondoka na ni jambo ambalo kwa kweli ukiliangalia linatia imani kidogo. Hawa watu wameshaondoka kazini au watu hawapaswi kupata mapato mengine kiasi ambacho kimebaki kwao ni hii pensheni ambayo inapaswa ilipwe kwao. Sasa wanapozungushwa, wanapoambiwa wana nyaraka, kwa sababu nyaraka na sisi tukubali kwa mfano mimi sasa ukiniuliza nyaraka zangu kwa mfano za Elimu ya Sekondari, naweza nikahangaika kuzipata, itanibidi labda niende kwenye shule nilikosomea. Maana yake sina. Sasa hii wengine wameshaondoka kazini wamejitahidi kutunza lakini sasa hawana. Hili jambo mimi ningeiomba sana Wizara na

Serikali, ilichukue kwa sababu napata malalamiko mengi, najua nikirudi Jimboni kule nitakuta malalamiko haya bado yananisubiri.

Sasa tungeomba hili lielezwe vizuri na Wizara iseme inalichukuliaje na italitekelezaje kwa Wananchi ili kila mmoja aweze kufaidika na hali hii halisi ya mapato na hati yake. Akienda basi aheshimiwe alipwe aondoke kwa sababu hakuna kitu kingine cha kufanya pale ni kufika anachukua malipo yake anaondoka. Mimi jambo hili ningeomba tulisimamie Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja tujaribu kuisisitiza Wizara iweke utaratibu mzuri zaidi ambao ni bora na rahisi kwa hawa wanaostahili kupata pensheni zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii na nimpongeze sana Waziri wa Fedha na Manaibu wote, kwa juhudi zao. Kwa kweli kuna mabadiliko makubwa ambayo tumeyaona wote, juhudi zao zinaonekana na unapokuwa na tatizo ambalo unalipeleka kwao kuhusiana na hoja ambayo unaiona ina malalamiko kutokana na Wananchi basi wanaichukua na kuiangalia kwa karibu na matokeo yake utayapata.

Mheshimwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia nami Muswada huu muhimu sana.

Lakini awali ya yote, ningependa kuungana na wenzangu walionitangulia na kutoa rambirambi zangu za dhati kwa kuondokewa na kipenzi chetu, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, ambaye alikuwa jirani yangu hapa. Baada ya kusema hivyo, ningeweza sasa kuingia kwenye mchango wangu wa Sheria ya Kodi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Wizara yake. Mabadiliko yanayotokea kila mara kwa kweli ni dalili ya uongozi wake bora katika Wizara hii ya Fedha.

Kwa upande wangu na Wananchi wa Musoma Vijijini, tunakupongeza sana kwa kutusikia kilio chetu kuhusu *windmill* na kwamba, mara moja umechukua nafasi yako muhimu na kuagiza marekebisho yafanyike na kwamba *windmill* sasa itakuwa ni *capital good* na zinaweza kuingia bila ushuru, nashukuru sana. Nadhani Wananchi wangu waliokuwa wananisikia walikuwa wanashangilia huko kwa vifijo kwamba wanapata maji bora baada ya mabadiliko haya kufanyika. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia kwamba niko *higher. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nakuja kwenye suala ambalo ni la aibu sana la *income tax. Income Tax Act* tuliipitisha mwezi wa nne, miezi mitatu iliyopita na mimi nakumbuka nilisema huu Muswada haufai. Kingereza kimekaa ovyo ovyo. Vijana wako Mheshimiwa Waziri, hawakufanya kazi nzuri. *Consultant* aliyefanya alifanya mambo ya ajabu ajabu. Nikasema sheria ya *income tax* ya mwaka 2004 itakuwa ni chanzo cha malumbano makubwa hapa nchini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika majibu yake siku hiyo, alisema mambo mazuri tutarekebisha baadaye. Miezi mitatu tunakaa hapa Bungeni kwenda kujadili mabadiliko, *amendment* kwa sheria ya *income tax* ya mwaka 2004, ni kichekesho kabisa. Tunakaa hapa tunalipwa posho ya Wananchi, kutunga sheria tena mwaka huu, sheria hiyo hiyo. Haya ni sawa kweli kwa walipa kodi wetu? Hii sheria iliyokuja sasa ya marekebisho pia ina matatizo, inataka kurekebishwa. Nisingependa kwenda mbali lakini nachukua nafasi hii nizungumzie tatizo la Watanzania wengi wanapopata makaridio ya kulipia *tax assessment.* Naomba nisome sheria mpya iliyoletwa hapa ambayo ni kama mabadiliko kwa ile iliyofanywa mwezi wa nne. Naomba ninukuu, *Section 12: "Any person who disputes an assessment made upon him may by notice in writing to the Commissioner General, object to the assessment".*

*Section 12 (4): "The Commissioner General may, upon being satisfied that there exist good reasons warranting reduction or waiver of tax payable in accordance with the requirement of subsection 3 direct that a lesser amount be paid or waive the required tax deposit". Commissioner* akipata *objection* yeye chini ya kifungu cha (12) (3) anaweza kukubali lakini atakubali tu, iwapo utalipa moja ya tatu. Ulipe moja ya tatu kabla hujasikilizwa kama kweli unachokisema ni kweli ama laa. Kama anakudai shilingi bilioni moja ni lazima ulipe milioni mia tatu na nusu kabla hajakusikiliza hata kama unasema mimi silipi, mimi ni *pensioner* sitakiwi kulipa kodi, ukipewa *assessment* na *Commissioner* lazima ulipe moja ya tatu hata kama ni makosa. Lakini wanakuja kifungu cha (5), *Commissioner: "On receipt of the notice of objection, the Commissioner General shall admit the notice of objection to assessment of tax or refuse to admit the notice of objection to assessment.* Kwa kifungu hiki anaweza kukataa ku-*admit* na akikataa maana yake ulipe zile, hata kama wewe ni *pensioner* lipa zile alizotaka. Lazima alipe. Kwa hiyo, *tax payer* kama ni Balozi, kama ni nani lazima alipe.

Halafu kuna kichekesho sasa kwenye *subsection 6, The Commissioner General shall not refuse to admit the notice of objection to assessment of tax unless, the notice does not comply with the requirement of sub section (1),(2) or (3).* Ukiangalia *subsection one* ya *section 12,* huwezi kushindwa ku-*comply, it doesn't make sense.* Tukiangalia pale *subsection 3(2),* inasema, *the notice shall contain,* pengine unaweza kushindwa kuorodhesha maelezo fulani fulani inawezekana. Lakini hiyo pia anaweza kukataa. Linalonipa kero mimi ni ile 6(b), *the notice does not raise any question of law or fact,* eti kama umesema mimi niko *time bad* kisheria *commissioner* ana madaraka sasa ya kuwa Jaji aamue kama kweli hiyo *objection under 6,* inasema *raised any question of law.*

Mheshimiwa Spika, Katiba inasema waziwazi kabisa chombo pekee cha kusema sheria imekiukwa ama vipi ni Mahakama, siyo *Commissioner* hawezi. Kuna *separation of power,* anaye-*determine a mass of law, in charge.* Sasa hapa imekiuka, nadhani anakiuka. Hii sheria tukipitisha inakiuka Katiba. Mwisho pengine anasema pengine (c) anasema kama unachoomba ambayo ni *the relief sought cannot granted in law.* Eti *Commissioner* anasema hizi sheria unachoomba kisheria haikupi, hii ndiyo nani, ni Jaji tu anaweza kusema unachosema sheria haikuruhusu, siyo *Commissioner.* Nchi zote wanaofanya hawafanyi hivi. Ni kazi mbovu itatuletea hatari kama tukipitisha mabadiliko

haya. Lakini pia anasema: *"If the relief sought cannot be granted in law or equity". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *equity* siamini hata *Commissioner* anajua maana ya *equity* ni nini? Ukimwambia Ndugu Kitillya aseme hii siyo *equitable,* siamini anajua *equity* yeye ni nini. Anayejua *equity* ni *court of equity,* siyo yeye. *TRA* siyo *court of equity,* kazi yake ni kutoa *assessment* lipa. Nadhani kuna matatizo hayo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kabisa kwa dhati muangalie *objection,* jinsi ya *treatment* ya *objection,* vinginevyo wafanyabiashara hawataweka hapa fedha. Lazima *regime* iwe *friendly.* Kama *tax regime* haiko *friendly,* haiwezekani na inaweza kuwa *friend* tu kama una kesi. Mimi nimeonewa ninapotozwa kodi ama laa, vinginevyo haiwezekani na ndiyo tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho naomba unipe maelekezo, sheria ikiletwa Bungeni tunaipitisha ni muda gani mnatakiwa kufanya *amendment?* Ni mwezi mmoja baada ya kupitisha, miezi miwili ama mwaka mmoja kama nchi zingine zinavyosema au pengine naomba maelezo pia.

**SPIKA:** Utayapata katika utaratibu wa Kanuni za Bunge, hakuna kipindi maalum kilichowekwa kwamba sheria ikishapitishwa isirekebishwe katika muda fulani, hatuna *provision* hiyo. Kwa hiyo, inaweza ikapitishwa leo ikarekebishwa katika *session* inayofuata bado itakuwa sawa sawa tu, ama siyo *Attorney General?*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ulichokisema ni sahihi kabisa na niongeze tu kwamba, kwa mujibu wa sheria inayosimamia tafsiri za nchi hii *interpretation* na *general clause act* inaongezea kusema kwamba, hata sheria ambayo imepitishwa na Bunge hili lakini haijaanza kutumika inaweza pia ikarekebishwa na Bunge hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunahifadhi dakika zako mbili tulizochukua endelea.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Ahsante sana kwa ufafanuzi huo mzuri sana. Nilitaka kuomba Bunge liurudishe Muswada huu nyuma kwa kuwa umeletwa mapema mno, lakini nadhani kwa maelezo hayo, sitasema hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini ningeomba sana, unajua tunapewa muda mfupi sana, ningeweza kuchukua muda mrefu sana kueleza matatizo ya Muswada mpya huu ni kama ule ule wa kwanza. Nadhani watu wako hawakusaidii, naomba wa- *pull up their socks.*

Kwa machache niliyosema hapa, naunga mkono kwa shingo upande.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2004. Kwanza na mimi pamoja na kwamba ni mara yangu ya pili kuongea katika Bunge hili la bajeti, lakini napenda nichukue nafasi hii, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo

langu la Bunda, kutoa salamu za rambirambi kwa familia na Wananchi wa Jimbo la Ulanga, kwa kufiwa na aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ulanga Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira na naomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba, naunga mkono hoja hii. Lakini ninayo mawili ambayo ningependa nichangie katika Muswada huu. Moja ni kuhusu kodi ya soda, nakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anawasilisha hotuba ya bajeti ya Serikali ilionekana katika vinywaji vyote ambavyo vimepandishwa kodi, soda ndiyo ilionekana kuwa na kiwango cha juu cha asilimia katika tozo la kodi kwa sababu iko zaidi ya asilimia 6.5 wakati vinywaji vingine ikiwemo *whisk, wine*, pamoja na bia hata zile za kutoka nje, ziko katika kiwango cha asilimia tano.

Hili wakati tunayapitia mambo ambayo tumeona kwamba ni ya msingi tuweze kuishauri Serikali, nililisema hili kwamba soda ni kinywaji ambacho anakitumia mwananchi wa kawaida kijiji si *luxury* kwamba, Serikali katika kurekebisha viwango vyake vya kodi katika mambo mbalimbali basi iangalie kwamba soda imepandishwa kiwango cha kodi kimekuwa juu sana na tukaomba kwamba Serikali ijaribu kupunguza na yenyewe iwe kwa asilimia tano.

Maelezo ya Serikali ilikuwa ni kwamba, kama wakipunguza kodi hii iweze kuwa asilimia tano, basi inawezekana ikafumua bajeti nzima ya Serikali. Lakini nadhani kwa kuangalia huu umuhimu wa Wananchi kwamba soda inatumika hata kwa Wananchi kule vijijini, wagonjwa mahospitali na kadhalika, nadhani kuna haja na sababu za kila namna kwamba, Mheshimiwa Waziri, uweze kuangalia angalau soda nayo ipunguzwe kodi iweze kulingana na vinywaji vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kuhusu Muswada huu wa Sheria ya Fedha ni kwamba, lengo la Muswada huu ni kuboresha ukusanyaji mapato ya Serikali na kwa jinsi ninavyoelewa mimi kodi yoyote ile huwa hailipwi kwa hiari, mara nyingi huwa ni kwa njia ya kuvutana. Sasa kama ikipatikana njia nzuri ambayo inawezekana ikawa ni namna nzuri ya kuweza kutoa kodi bila kuwepo mvutano kati ya walipa kodi na mkusanyaji. Nadhani ni vizuri tukaishauri Serikali kama wanaona haja wakaitumia ili kuweza kuongeza ukuzaji wa pato la Serikali. Sasa ninao ushauri mmoja kwamba, kwa mfano, kwenye ada ya kuandikisha gari mtu, akitaka kuandikisha gari kama ndiyo analileta nchini analipa shilingi 95, 000/=, lakini mimi ninavyoelewa Watanzania wengi wana uwezo, kwamba wana fedha nyingi, wapo ambao wana kipato kikubwa na hili nalisema nimeliona katika nchi ya jirani nchi ya Uganda.

Wenzetu wa Uganda wameanzisha namba maalum ya magari, kwa wale watu wenye uwezo na ambao wanajisikia kwamba, wanataka waweze kuwa na namba hiyo maalum, unakuta mtu kwa mfano badala ya kulipa shilingi 95,000/=, Serikali inaweza ikapanga kwamba, kutakuwepo na namba maalum ya gari ambayo kwenye gari itaandikwa jina la mtu badala ya *plate* namba. Lakini kodi hiyo, inabidi iwe juu zaidi, hicho kiwango cha kupata hiyo namba maalum, kwa nchi yetu inawezekana labda watu wakaambiwa kwamba, mtu anaweza akalipa shilingi milioni moja halafu na gari lake

likawa na jina lake. Kwa mfano, mimi hapa Nyaburi badala ya kuwa namba mfano, ADY sijui ngapi ngapi unakuta labda *plate* namba ya gari yangu imeandikwa Nyaburi kwa sababu nitakuwa nimelipa kwa kupenda kwangu na kwa kuzingatia uwezo wangu mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Sasa nadhani njia hii inaweza ikawa ni bora zaidi itakuza Pato la Taifa kwa sababu kwa wale wenye kujisikia wenye uwezo ninaamini wanaweza wakafanya njia hii nayo itachangia kukuza pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda nikuombe kupitia kwako kwamba, Serikali isione kigugumizi kupitisha labda kubuni mpango huu kwa sababu hata sasa tunaona Waheshimiwa Mawaziri, unakuta gari imeandika Naibu Waziri labda Sayansi na Teknolojia unaona *NW ST* tunaona labda *Chief Secrectary,* tunaona labda gari la Jaji Mkuu na haijaathiri chochote.

Kwa hiyo, napenda nishauri Serikali kwamba, Serikali kama inaona mpango huu labda inaweza kuwa na mashaka nao, wenzetu wa Uganda tuko nao kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, nadhani tutumie fursa hii basi tujifunze, labda tuongee nao wenzetu kwamba ni utaratibu gani wanaotumia na kwamba tunaweza kujifunza ni jinsi gani wanavyoendesha mpango huu na mpango huu pia sisi tuuanze hapa kwetu Tanzania kwa wale Watanzania watakaokuwa wana uwezo na wanaona kwamba, wana fedha za kutosha, mimi naamini wengi watajitokeza na kuweza kuwa na namba maalum za magari ambazo zitaandikwa majina ya watu binafsi, wamiliki wa vyombo hivyo vya usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kweli sina mengi, nakushukuru sana lakini naomba Mheshimiwa Waziri, uzingatie hili mjaribu kulifanyia kazi kwa sababu lengo ni ku-*improve* mapato ya Serikali. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, Serikali ilikubali ushauri wa Kamati wa kutaka *pipes for irrigation, cellular plastics sheets, soils,* ziingizwe moja kwa moja kwenye *General Tariff.* Hii haionekani kwenye *schedule of amendments* ilivyowasilishwa asubuhi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni kwa nini Serikali imegeuza msimamo wake nje ya muafaka tuliofikia? Muafaka huu ulifikiwa baada ya kuzingatia umuhimu wa bidhaa hizi kwenye Sekta ya Kilimo kwa sababu Bajeti hii imeweka mkazo kuisaidia Sekta ya Kilimo. Napenda kuishauri Serikali irejee msimamo wake kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* kuna malalamiko ya kufukuzwa kazi watu kwa uonevu, Kamati iliyopendekezwa na Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ichunguze pia na kesi ya mtumishi mmoja aliyefukuzwa

*TRA* anayeitwa Juma Kimwaga, yeye alikuwa chini ya Msaidizi wa Kamishna. Kijana huyo alikuwa katika Kitengo cha Misamaha ya Kodi, inasemekana amegandamizwa kufukuzwa kwake. Kamati au Tume Huru iundwe kwa kesi yake ili kuondoa manung'uniko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni hitimisho la zoezi zima la Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005.

Baada ya hotuba zote na maombi ya fedha zote, sasa Muswada huu unahitimisha na kuweka utaratibu wa kuzikusanya fedha hizo ili zipatikane. Hoja zile za Wizara zilizowasilishwa hapa kwa nyakati tofauti ni malikauli. Huu Muswada wa *Finance Bill* ndiyo unaweka utaratibu wa kuzipata fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu ni kwamba, Wizara ijipange vizuri kama ilivyo, hata ikabidi tuombe Malaika toka Mbinguni kuongeza nguvu. Wananchi nao waelimishwe kuwa tulifanya maamuzi makubwa, mazito, mazuri ya kuthubutu kufuta kodi kero 60, kodi ya maendeleo, mifugo, ushuru, *UPE* na kadhalika. Haya ni mafanikio. Sasa tulipe kodi kwa maendeleo ya Taifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji waliokuwa wamejiandikisha kwa Muswada huu wamemalizika. Kama kawaida yetu sasa tutawapa watoa hoja nafasi ya kwenda kuandaa majibu ili yatolewe kipindi cha mchana tutakaporejea pamoja na kuendelea na hatua zilizosalia za kupitisha Muswada huu. Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.22 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ya Muswada wa *Finance Bill* wa mwaka 2004 ambao ni wa aina mbili, wa kwanza waliochangia kwa maandishi ni wawili tu. Mheshimiwa Felix Mrema, Mbunge wa Arusha na Mheshimiwa Tembe Nyaburi, Mbunge wa Bunda, ambaye pia baadaye alichangia kwa kusema kwa maneno. *(Makofi)*

Vilevile niwashukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Msemaji wa Upande wa Upinzani, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Muttamwega Mugaywa na Mheshimiwa Philip Marmo, katika kuboresha Muswada wenyewe. *(Kicheko)*

Kwa upande wa Kamati ya Fedha labda niwashukuru sana kwa uelewa wao na kwa kuunga mkono Muswada wenyewe kwa sehemu kubwa. Niseme kwamba katika majadiliano kwenye Kamati kama alivyosema mwenyewe, kuna mambo ambayo niliahidi kuyafuatilia. Moja linahusu zile kodi wanazotozwa wafanyabiashara wadogo wadogo zilizoko kwenye *schedule* ya Muswada huu na zile kodi wanazolipa kwenye ile *schedule* nyingine ya wafanyakazi kuangalia uwiano na *harmonization.* Hilo nitalifanyia kazi na vilevile hili suala zima la kodi kwa wafanyakazi iweje kwa siku zijazo. Kama nilivyosema hili nitalifanyia kazi kwa mwaka huu na tutakuja tena labda na maamuzi au mapendekezo ambayo tutajadiliana tena baadaye.

Kwa upande wa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, niseme kwamba, wasiwasi wake wote umekwisha kwa sababu suala lile la uhakika wa *self assessment* kwamba kama watu wanajikadiria kodi wenyewe, itakuwaje, tutawadhibiti namna gani na tutajuaje kwamba hawadanganyi, dhana yenyewe ina utaratibu na huu utaratibu uko kwenye *regulations,* kwenye Kanuni zilizotungwa kwa sababu hiyo na tunajua kwamba nchi nyingine zinafanya kazi kama hizo na kwa hiyo kwa hapa tutajaribu kutumia mbinu kama hizo. Lakini ni kweli kwamba, lazima tuwe waangalifu sana kwa sababu watu wanaweza wakadanganya na kutuharibia mambo. Kwa hiyo, hilo tunalo na tumejiandaa kulikabili. Hili la *One Stop Centre* tayari nimelisema hata kwenye hotuba yangu jana kwamba, tumekwishaanza utaratibu huo wa kazi zote za Mamlaka kufanyika kwenye Ofisi moja. Ndiyo hiyo *One Stop Centre*, kazi zote za *VAT, revenue,* isipokuwa zile za forodha kwa sababu sio kila mahali pana forodha. Kwa hiyo, tumeanza na tunataka utaratibu huu uimarishwe ili kupunguza watu kusumbuka kama alivyohofu Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

Kuhusu uhusiano wa Walipakodi na Mamlaka, hilo tayari nimeshalieleza mara nyingi hapa, tunaendelea kujenga uhusiano huo. Hivi sasa kila mwezi Mamlaka inakutana na Walipakodi hasa wale wakubwa na kusikiliza malalamiko yao, mapendekezo yao, namna ya kujenga mahusiano mazuri baina yao. Hili ni wazo muhimu na tunalo na ni sehemu ya kazi yetu.

Mwisho, kutafsiri sheria kwa Kiswahili ni wazo zuri sana ila kama nchi bado hatufanyi kazi hii vizuri sana, hili ni wazo ambalo labda nitalijadili na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona tunafanyaje. Tatizo la kutafsiri kwa Kiswahili ni kwamba, ile tafsiri ikifanywa vibaya, kwenye Mahakama kutatokea matatizo makubwa sana kwa sababu neno lililokuwa kwenye Kiingereza linaweza likatafsiriwa visivyo, kwa hiyo ukiendesha kesi kwa Kiswahili ukapata aina fulani ya tafsiri na ukiendesha kesi kwa Kiingereza ukapata aina nyingine ya tafsiri, nadhani ndio Wanasheria wanaogopa sana. Lakini ni wazo ambalo jibu lake mimi siwezi kulifahamu, ila ni wazo ambalo naweza nikalijadili na Mwanasheria Mkuu wa Serikali tukaona tufanyeje.

Mheshimiwa Job Ndugai, alikuwa na mawazo mazuri na tunamshukuru sana kwa kutupa moyo Wizara na Mamlaka ya Mapato. Niseme tu wasiwasi wake juu ya kile Kifungu cha ile Sheria ya 72, haupo kwa sababu tumesema hapa kwamba, Kifungu cha nane kimefutwa, *Section* (h), inafutwa. Kwa hiyo, hiyo inaondoa ule wasiwasi ambao alikuwanao Mheshimiwa Job Ndugai. Ile *schedule* inabaki vilevile kwa maana ya aina ya

biashara isipokuwa *rate* zinabadilika kama ilivyo kwenye aya za (a) na (b). Kifungu cha tisa kinaweka utaratibu mpya wa nani atakusanya nini na biashara hizi hazitahitaji leseni. Lakini niko tayari, hata jana nilisikia wasiwasi mwingine wa aina hiyo, niko tayari kama kukitokea matatizo huko Vijijini au kwenye Majimbo yetu kusikiliza matatizo haya yako wapi. Ninavyoelewa mimi hadi leo Watendaji walikuwa hawajui wafanye nini kwa sababu sheria ilikuwa haijapita, lakini tumaini langu ni kwamba, baada ya sheria hii kupita na Rais akatia saini, Watendaji watajua kwa uhakika kabisa nini wanatakiwa kufanya kuhusiana na sheria hii ya mwaka 1972 na sheria nyingine zote nilizoainisha hapa kwamba, zinafanyiwa marekebisho. Tumaini langu ni kwamba, hili tatizo halitakuwepo tena.

Kuhusu suala la misamaha ya kodi kwa Madiwani, lilizungumzwa na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa. Nijuavyo mimi, Madiwani hawana mshahara. Madiwani wanaishi tu kwa posho. Kwa hiyo, kama Diwani yeyote anastahili au anahitaji msamaha wa kodi, itabidi iwe kwa mazingira mengine sio hayo ya Udiwani. Kama mnavyojua Serikali kwa ujumla wake haipendi sana siku hizi kusamehe kodi, lakini kama kuna sababu za misamaha kwa misingi ile ambayo iko kwenye sheria kutakuwa hakuna tatizo lolote kabisa.

Mheshimiwa Philip Marmo, alikuwa na wasiwasi juu ya malipo ya pensheni. Kwanza, niseme moja kuhusiana na hali ilivyo leo au wiki hii ya malipo ya pensheni na mishahara nchini. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, sisi katika Hazina tutahakikisha kwamba, ikifika tarehe 25 fedha zimeshatoka Hazina kuelekea Mikoani, zilipwe kwa wakati. Hiyo nimeisema hata kwenye hotuba. Kwa hiyo, hatutegemei kwamba, kutatokea matatizo ya malipo ya mshahara huko Wilayani na kama yakitokea ni matatizo ya huko huko, hayatakuwa matatizo ya Hazina kwa sababu hata siku moja hatujakosa uwezo wa kulipa mshahara ili watu hata wawe na wasiwasi kwamba labda kipindi hiki Serikali imekosa fedha. Hilo halipo! Kwa hiyo, likitokea tatizo litakuwa huko.

Lakini wiki hii Waheshimiwa Wabunge, niombe radhi kwamba, wale wanaostahili kulipwa pensheni zao za kawaida wamepata matatizo kidogo kwa sababu tunabadili utaratibu ili wastaafu wanaolipwa pensheni waweze kulipwa kupitia Benki ya *NMB*. Uamuzi huo ulifanywa halafu ukakumbwa na matatizo ya kiutawala kati ya Benki Kuu, Wizara ya Fedha na Benki ya *NMB*. Lakini leo wakati wa mapumziko ya mchana nilikuwa na mazungumzo na Meneja Mkuu wa *NMB* na Mwenyekiti wa *NMB* hapa Dodoma na wamenihakikishia kwamba, hilo tatizo ni kama limekwishapatiwa ufumbuzi, watu wamechelewa kidogo labda siku moja au mbili, lakini kwa sababu jambo hawajalizoea linawashangaza wengine kwa nini twende Benki, lakini halitarudiwa, ni jambo tu lililotokea kutokana na *switchover.* Kwa hiyo, kwa usumbufu huo kwa kweli naomba radhi, ni kwa sababu tunataka mishahara na pensheni zote zilipwe kupitia Benki. Hiyo ndiyo dhana tunayotaka kujenga.

Sasa hili la wasiokuwa na vithibitisho ambalo ndilo Mheshimiwa Philip Marmo, alikuwa na wasiwasi nalo, ningependa niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tutajitahidi kwa kila njia halali kuhakikisha kwamba, hakuna mstaafu wa mkupuo

atakayekoseshwa malipo yake kwa sababu tu *documents* zake zilipotea, hiyo haitatokea. Tutautumia kila njia halali na moja ni kuwapa kama alivyopendekeza Mheshimiwa Philip Marmo, lakini nyingine ni *identification.* Inawezekana kuna ushahidi wa aina nyingine labda kuna mtawala fulani pale au mzee au nani anaweza akasema huyu ni fulani na kadhalika. Tunalochunga sisi kusitokee wizi, kusitokee wanadeni hewa. Kwa hiyo, hilo ningeomba mtuamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mapato ya leseni kama nilivyosema watakaofidiwa ni Wizara ya Biashara ambayo ndiyo ilikuwa inafaidika na leseni hizi. Lakini tumaini langu ni kwamba, hakutatokea vurumai zaidi kwenye jambo hili kwa sababu sidhani kama kuna Halmashauri nyingi sana ambazo zilikuwa zinategemea sana leseni.

Labda nizungumzie habari ya hizi kodi za wafanyakazi. Ni kweli kwa kupandisha kiwango cha chini cha mshahara kutoka Sh.50,000/= mpaka Sh.60,000/=, wafanyakazi watakuwa kwa kiasi fulani wamepata nafuu hawa walio chini ya Sh.60,000/=. Lakini ukizidi kupandisha ukaenda juu zaidi maana yake itakuwa sio kwa wafanyakazi wa Serikali tu, itakuwa sasa na wafanyakazi wengine na kama Mheshimiwa Mbunge mmoja alivyosema kwenye Kamati ya Fedha kwamba, eneo la wafanyakazi ni chanzo kikubwa sana cha kodi kwa Serikali. Kwa hiyo, tutakapofika kufikiria hoja hii kwamba wafanyakazi wanalipa kodi zaidi na kadhalika, itabidi vilevile tufikirie njia za kufidia endapo tutafanya uamuzi wa namna hiyo. Kwa hiyo, ni kati ya mambo niliyosema nitachunguza.

Kulikuwepo na swali nadhani la Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa kwamba, kwa nini Serikali isitoe unafuu wa kodi kwa watu wadogo wanaofyeka mashamba, misitu na kadhalika. Lakini kodi hizi zinatolewa kwenye mapato. Ni kodi ya mapato kwa sababu ndio kodi tunayoitambua kwenye eneo hili. Kwa hiyo, kama ni kodi ya mapato, huyo mtu atafuata tu taratibu zilizopo kama nilivyoeleza hapa mwanzo na atapata msamaha wake.

Sheria ya Mapato ya Mwaka 2004 ni mbaya, imeandikwa vibaya, ina mambo yasiyofaa na kwamba ni ajabu kwa nini tunaanza kuibadili. Ningependa niseme tu kwamba, sheria yoyote ile ni *dynamic*, hakuna sheria iliyoganda, inakaa tu pale imeganda. Haiko! Kwa hiyo, kila siku likitokea jambo jipya lazima tubadilishe sheria ili ku-*accommodate* jambo hilo jipya. Lakini ya pili, hata wakati nilipokuwa nawasilisha Muswada wa Sheria hiyo hapa, sikusema kwamba sheria hii ni *perfect,* hapana! Sheria hii ni *workable.* Nilisema sheria hii inaweza ikatumika, ni *workable,* lakini tunajifunza kama tunavyozidi kubadilisha mambo na kubadilika sisi wenyewe tunajifunza na lazima tubadilishe hiyo sheria.

Kulikuwa na wazo kwamba, tuangalie maeneo mengine kwa mfano, ya *internet* tuyapige kodi na kadhalika. Eneo zima hili la *IT* matumizi ya teknolojia ya kisasa ya mitandao ni eneo ambalo ni changa sana kwa kweli hapa Tanzania na kwa sababu hiyo tunakuwa waangalifu sana kabla ya kuweka kodi mahali kwa sababu tunaweza tukadumaza lile eneo badala ya kulifanya likue na ndiyo maana nilikazana miaka mitatu

iliyopita kuomba Bunge kwamba, tupunguze ushuru kwenye *computer* kwa sababu msingi wa haya ni *computer* na mlikubali na tutaendelea kusisitiza kwamba, tuendelee kupunguza hizo kodi kwenye kompyuta mpaka hapo tutakapoona kwamba, labda teknolojia hii sasa inafurika na imetengamaa. Kwa hiyo, ndio tunaingiza mkono pale kidogo wa kodi kwa kuvuna kile tulichopanda. Kwa hiyo, sasa hivi tuko kwenye kupanda, hatujafika mahali pa kuvuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme vilevile kuhusiana na suala la gesi. Gesi ya Songosongo mimi naliogopa sana kuanza kui-*tax* hata kabla hatujaitumia. Hii ni sawa na kununua nepi kabla mtoto hajazaliwa. Kwa hiyo, wazo hili lilipokuja nikasema hapana, tujipe mwaka, tujue hii gesi itakuwa ni kitu cha namna gani, italeta matatizo gani, itawafaidisha namna gani hao watakaoitumia kabla hatujaweka kodi yoyote pale. Vilevile tulishauriwa na wataalam kwamba, tusipoangalia, watu wanaweza wakakataa kutumia hii gesi wakaendelea kutumia aina nyingine za nishati kama *Industrial Fuel Oil.* Kwa hiyo, tunakuwa waangalifu tusianze kuvuna kabla hatujapanda. *(Kicheko)*

Huu udhibiti wa misamaha ya kodi kwenye vipuli, niseme tu kama nilivyokuwa najibu hoja ya Mheshimiwa Felix Mrema, leo Mheshimiwa Felix Mrema ameniletea tena wazo lingine kwamba, katika mambo haya kuna vitu vingine ambavyo ni vigumu sana kusema unavisamehe kwa sababu ya kilimo kumbe unaweza ukafumua mambo yasiyofaa. Kwa mfano, Mheshimiwa Felix Mrema, tumekuwa tukizungumza naye juu ya *plastic sheets* kama vyandarua hivi vya *plastic* ambavyo wanatumia sana kwenye kilimo cha maua. Ukishasema *plastic sheets* zinasamehewa kwa ujumla wake, huna uhakika kama zimekwenda kwenye maua au zimekwenda kwenye aina nyingine za majengo. Kwa hiyo, sikuileta hapa kwa sababu ni lazima iwe *specific* niseme hii ni kwa ajili ya kiwanda fulani kilichoko mahali fulani, naiweka kwenye *General Notice (GN).* Kwa hiyo, kuna mambo mengine mengi tu ambayo nitayaweka kwenye *GN* kwa sababu ya kuogopa kwamba ukifumua kwa ujumla wake, wengi wanaotaka kukwepa kodi watatumia muda huo kukwepa kodi. Lakini wazo la Mheshimiwa Felix Mrema, tunalo na tutalishughulikia kwa utaratibu huo na kuna bidhaa nyingine chache ambazo tutaziingiza kwenye utaratibu wa *GN* badala ya hii ya *Finance Bill.*

Labda sasa nirudi kwa mzee wangu Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ni mwenzangu wa siku nyingi sana. Mimi nilikuwa Mkurugenzi Mkuu wa *SIDO* na kwa kutambua uwezo aliokuwanao Mheshimiwa Stephen Kahumbi siku hizo nikamteua kwa hiari yangu kabisa na kwa moyo safi kuwa Mkuu wangu wa Mkoa wa Tabora na alifanya kazi nzuri na leo tuko hapa tunaendelea kufanya kazi nzuri pamoja. Palipo Mheshimiwa Stephen Kahumbi na mimi, haliharibiki neno. Hilo nataka mfahamu kabisa. *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mkuu wa Wilaya!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mkuu wa Mkoa wa *SIDO* sio Mkuu wa Serikali. *(Kicheko)*

Lakini kwa leo, kwa mara ya kwanza, kama vile Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ameleta jambo hapa Bungeni la aina hii aliloleta na mimi kwa mara ya kwanza

nitashindwa kukubaliana naye. Kwa mara ya kwanza toka miaka ya 70, nitashindwa kukubaliana naye. Kwa nini nashindwa kukubaliana naye?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge katika kila Kikao na maswali mengi yanayohusu Mamlaka ya Mapato na Kodi mnaendelea kusisitiza umuhimu wa kutokukwepa kodi, kudhibiti wakwepa kodi na kuhimiza umuhimu wa kukusanya kodi yote, mnaendelea kuhimiza umuhimu wa watumishi ndani ya *TRA* walio waadilifu na wanaofanya kazi waliyotumwa ya kukusanya mapato halali ya Serikali. Hayo ndiyo mnatusisitizia na mimi nimesema mara nyingi kwamba, inapokuja mtu anatifua mwelekeo huo wa kusaidiana na watu kuibia Serikali mapato, kukwepa kodi, mimi siwezi kuingia kwenye mkondo huo. Siwezi kabisa! Sasa kuna watumishi wawili. Kesi hii ni ya mwaka 2001, sio ya leo. Tarehe hizo hata Kamishna wa sasa wa kodi alikuwa hajaajiriwa kwenye Mamlaka hiyo, walikuwa watu wengine.

Hadithi ni kwamba wako watumishi wawili, mmoja anaitwa Agnes Mkemwa, ndiye huyu ambaye ametajwa hapa leo na mwingine anaitwa Jackson Mutoka. Watumishi hawa walikuwa kwenye Ofisi ya Mamlaka ya Mapato Mbeya. Watumishi hawa walituhumiwa na kushitakiwa na kukuta wana kosa kwa utaratibu wa Sheria za Kazi kwamba, wana makosa ya kushirikiana na watu waliokuwa wanakwepa kodi za *VAT* kutokana na ununuzi wa mabati. Kilichotokea ni kwamba, kulitoka kisingizio kwamba kuna Kanisa linaloitwa *Church of Priest* Mbeya na Ileje kwamba, Kanisa hili lilikuwa linaomba msamaha wa mabati 3,520, msamaha wa kodi ya *VAT.* Kwamba, watumishi hawa wawili wa *TRA* kule Mbeya walishirikiana wakatoa msahama huo kwa kutumia karatasi za msahama zilizokuwepo kule Mbeya. Msamaha wa kodi hii hautolewi na mtumishi yeyote ambaye hakutajwa kwenye sheria.

Watumishi hawa mmoja anayeitwa Jackson alikuwa na cheo cha *Financial Management Officer* na huyu Agnes alikuwa *Assistant Financial Management Officer.* Hawa hawana Mamlaka Kisheria ya kutoa kibali chochote cha msamaha wowote wa kodi. Kama mnavyojua, hata mimi Mamlaka niliyokuwanayo, mlikuja kunipunguzia hapa kwa sheria niliyowasilisha hapa mimi mwenyewe mwaka 2003 kwamba hata Waziri wa Fedha adhibitiwe wakati anapotoa misamaha na kwamba misamaha hiyo iwe ndani ya sheria au kama sio ndani ya sheria, ifuate utaratibu fulani mpaka hapo Waziri mwenyewe atakapotoa huo msamaha. Ndio sheria tuliyopitisha hapa. Hata wakati huo kulikuwa hakuna mtumishi wa ngazi ya chini katika Mamlaka aliyekuwa na uwezo wa kutoa msamaha wa kodi ya *VAT.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna karatasi hapa nitakupa baadaye, tunao ushahidi hapa wa maandishi kwamba, watumishi hawa walisaini karatasi za kutoa msamaha kwa Kanisa hili. Mabati haya yalichukuliwa kwenye Kampuni mbili, *ALAF* haya yalichukuliwa na moja kwa moja hatujayaona na Kampuni nyingine inaitwa *J.J. Industries.* Hayo yalichukuliwa na tumeyakamata toka mwaka huo wa 2001, tunayo kwa sababu kuna kesi Mahakamani na yale mabati ni ushahidi. Katika uchunguzi watu wazuri kule Mbeya wakatuambia kuna magendo yanaendelea hapa miongoni mwa watumishi wenu nyie Mamlaka na wafanyabiashara kule Mbeya. *TRA* walipopeleka

wachunguzi wakagundua kwamba, ni kweli jambo hilo lilifanyika na ni kweli kulikuwepo na hali hiyo.

Aliyekuwa anatumika ni mtu mmoja anaitwa *Reverend* Edwin Tusekelege wa hilo Kanisa ndiye aliyepewa hicho kibali. *Reverend* Edwin Tusekelege wa hilo Kanisa kwa maandishi aliyotoa hapo ninayo, alikanusha akasema mimi ni kweli nilikuwa naomba kibali lakini sijapewa mabati, mpaka leo nasubiri na sijui ni nani alipewa na nani alichukua. Kwa hiyo, baada ya uchunguzi ikabidi sasa kutokee ushahidi na maelezo. Nitakusomeeni barua iliyoandikwa na Mamlaka wakati huo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ikisema: "Kufukuzwa kazi kwa Bibi Agnes Mkemwa wa Mbeya." Maana huyu ndiye alikuwa analalamika zaidi. Anasema: "Tulipata taarifa, halafu akasema, baada ya kupata taarifa hiyo ikiwa ni pamoja na kutajwa sehemu ya tukio, tuliwatuma Maofisa wetu kwa ajili ya ufuatiliaji na uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi huu yalithibitisha tuhuma hizo baada ya kumnasa mtu mmoja mwenye kibali cha unafuu wa kodi kutoka Ofisi ya *VAT* Mbeya aliyenunua mabati 3,520 kutoka *J.J. Industries."* Kwa mujibu wa Ankara hizo, huyu bwana alikwenda kununua kwa jina la Kanisa la Kristo Ileje Mbeya ambalo sasa kama nilivyosema, walikanusha. *(Kicheko)*

Wanasema: "Aidha, kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja kabla, Kanisa hilo lilidaiwa lilikuwa limepewa kibali kingine kutoka Ofisi hiyo ya *VAT* Mbeya cha kununua mabati 8,000 kutoka *ALAF* bila ya *VAT.* Mabati hayo tayari yalishachukuliwa na kodi ya Sh.5,458,300/= imepotea moja kwa moja." Huu ni uchunguzi. Katika vibali vyote viwili Maofisa waliohusika ni Bibi Agnes Mkemwa na Bwana Jackson Mutoka, ambapo jumla ya kodi iliyosamehewa kwenye vibali hivyo vyote viwili ni Sh.7,878,300/=.

Kwa hiyo, katika sura hiyo kukaanza sasa kutokea migogoro na hawa watumishi wakafukuzwa kazi wote wawili na Mamlaka ya *TRA.* Hadithi ni ndefu, ikapita kwenye utaratibu wa sheria ya kazi. Ikafika mahali kama alivyosema Mheshimiwa Stephen Kahumbi, katika utaratibu huo, Waziri wa Kazi akaamua kwamba, huyu mtumishi ingawa alikosea lakini adhabu mliyompa ni kubwa, akaamua kwamba arudishwe kazini. Ile sheria ina kipengele kinasema Waziri wa Kazi anapotoa hukumu yake, Mwajiri anaweza akafanya nini, mwajiri anaweza akatekeleza au naye kwa mujibu wa sheria hiyo hiyo akafanya kitu kingine, akamwachisha kazi na kumlipa mafao.

*TRA* wameeleza hivi: *"Where a reinstatement or reengagement has been ordered under this section,* yaani hii *section* ya sheria ya usalama kazini *and the employer refuses or fails to comply with order.* Anasema: *"The employer shall be liable to pay the employee compensation of an amount equal to the aggregate of one the statutory compensation computed in accordance with section 35 and to a sum equal to 12 months wages at the rate of wages to which the employee was entitled immediately before the termination of this dismissal".*

Kwa hiyo, Mamlaka ika-*opt* kwamba, hawa watu kwa sababu wali-*collude* na watu wa nje kupoteza mamilioni ya fedha kwa udanganyifu kwa kutumia nafasi zao ofisini, watu hawa hatuwezi kuwaweka tena kwenye Mamlaka. Kwa hiyo, badala yake, kwa heshima na taadhima, pamoja na uamuzi wa Waziri wetu, hawa waondoke na

tutawalipa na wamelipwa. Wamekwishalipwa Shilingi zaidi ya milioni sita, huyu mama, sio wote wawili.

Huyu mama amekwishalipwa Shilingi zaidi ya milioni sita baada ya Shirika kushindwa kumpokea tena kazini na hakuna sheria inayosema kwamba, Waziri akiamua Idara zote za Serikali na vyombo vya Serikali lazima vimtii Waziri, hakuna sheria ya namna hiyo.

Mimi niliwahi kuwa Waziri wa Kazi na hukumu hii mimi nilikuwa naitumia. Waziri anapokaa pale hakai kama Waziri, anakaa kama Mahakama na Mahakama ile ina utaratibu wa rufaa na inampa mwajiri ruhusa ya kutii au kulipa. Hawa wameamua kulipa. Kwa nini wamelipa? Wamelipa kwa sababu mchezo huu ulikuwa unachezwa sana ndani ya *TRA* na hii ilikuwa labda arobaini tu hawa wamekamatwa.

Kwa hiyo, wakasema hawa tuwakamate tuwaonyeshe mfano kwa wengine. Ya pili, kama ukiwarudisha kazini wale wengine wanaofanya mchezo huo, watasema oah! Kumbe unaweza ukafanya mambo yako, ukaenda huko ukarudishwa kazini. Kwa hiyo, wangeendelea na mchezo badala ya kuchukua ile kama ni mfano mbaya. Kwa hiyo, Mamlaka ikaamua hivyo.

Huyu mama alipopokea siku ile alipoamua kupokea malipo haya ya shilingi milioni sita, ndiyo siku aliyokata rufaa, ndiyo siku aliyomaliza kesi yeye mwenyewe. Siku ile alipopokea tu ndiyo siku aliyojihukumu mwenyewe. Kwa hiyo, ilikuwa hakuna tena kesi. Sasa inakuwaje, wewe umepokea kwa kukubali kwamba, ulifanya kosa na umeshalipwa kulingana na Sheria kisha unarudi unasema Mbunge nitetee nirudishwe kazini. Maana mgogoro hapa ni kurudishwa kazini. Nimeshapokea nimeweka mfukoni. Sasa Mbunge nisaidie nirudishwe kazini. Mbunge kweli akajitahidi wala sitegemei Mbunge awe Mwanasheria ajue *technicalities* zozote, haya mimi nayasema kwa sababu nina fursa zaidi kuliko Mbunge.

Mbunge akaja, toka mwaka 2003 nimezungumza na Mbunge. Nikamwambia Mbunge, mimi unanielewa ni mtu wa haki. Ngoja nichunguze nijue kilichotokea ni nini. Ndiyo nikapata makaratasi yote haya. Nikarudi kwenye Mamlaka, nikamwambia Mamlaka sasa hata kama ilikuwa ni chuki, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, mnaonaje sasa hivi toka mwaka 2001. Mwenyekiti wa *TRA,* Dr. Bukuku ananiambia hawa walipewa *same treatment* hapakuwa na ubaguzi wa aina yoyote.

Mmoja amerudi kusema anataka kurudi kazini. Mwingine amekubali amenyamaza huko aliko. Je, tunatoa picha gani kwa vita dhidi ya wakwepa kodi na wale watumishi wa *TRA* wanaosaidiana na wakwepa kodi kwa kumrudisha huyu? Alinijibu huyu Mwenyekiti. Bodi ya *TRA* inaona siyo busara kutetea watumishi wabovu na wenye makosa. *TRA* inaona kuwa pamoja na uamuzi wa Waziri na malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge haya ya leo na yale ya juzi, *option* ya kuwalipa watu hao na kuachana nao kabisa ndiyo sahihi kwamba, hawakudhulumiwa kabisa. Kuwarudisha watu hao itakuwa mbaya kwa watumishi waadilifu wa *TRA* na wanaojua makosa ya watu hawa. Aidha, kuwarudisha watumishi hawa kutawadhoofisha na kutawavunja moyo *management*

wanaosimamia kazi ngumu ya kukusanya mapato na kusimamia nidhamu na maadili ya kazi.

Kwa hiyo, mtazamo wa *management* ya *TRA* pamoja na Bodi ni kulinda *TRA's best interest* na *best interest* ni kutowahurumia wanaosaidiana na watu wa nje kukwepa mamilioni ya fedha za *VAT*. Kuwarudisha watu hao itaathiri sana *TRA* na kwa hiyo msimamo wa Bodi na *management* ni huo; hakuna mtu aliyeonewa pamoja na huyu mama. Lakini kwa bahati mbaya sana Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasikitika sana kwamba, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, amelalamikia barua iliyoandikwa kwake. Hata mimi nilishtuka sana kwamba, inakuwaje watu wanamwandikia Mheshimiwa Mbunge barua namna hiyo.

Hata mimi nilishtuka alivyokuwa anaeleza Mheshimiwa Stephen Kahumbi, kumbe sivyo. Hawa baada ya mizunguko yote hiyo juzi tarehe 2 Agosti, wakamwandikia tena hawa watu. *TRA,* wakamwandikia tena huyu Mama Agnes kwamba, mama tulishakulipa na Sheria ndiyo hiyo, wakamwonyesha hii Sheria, kisha na wakamwambia tunakushauri usiendeleze tena jambo hili kwa sababu halifai, maana barua hiyo ndiyo ya tarehe 2 Agosti walimwandikia huyu mama, ndiyo walionakili kwa Mheshimiwa Mbunge na ndiyo waliyonakili kwangu Waziri kusema jambo hili tumelifikisha hapa, nia yao ilikuwa uwazi. Mbunge ajue na Waziri ajue siyo kwamba, walikuwa wanataka kumfuatilia Mbunge huku Bungeni.

Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, kwenye *Hansard* ni kweli alisema atafuatilia hili jambo lakini hakutoa *interpretation* ya kisheria, alisema tu atafuatilia hili jambo ajue sasa kumetokea nini. Mambo haya ya Mawaziri tunasaini mambo mengi, hujui kukumbuka moja moja. Kwa bahati mbaya sijapata fursa ya kuzungumza na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, hata pia kama tungezungumza na Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, anaielewa hii Sheria. Anayaelewa haya ninayoyasema, kwa sababu hatukuzungumza lakini ukweli ndiyo huo, ila huyu mama amefika mahali akasema basi namalizia. Anaandika barua kwa mkubwa wake tena tarehe 28 mwezi wa saba na alinakili kwangu vilevile na mimi sikuona ajabu alinakili kwangu na alikuwa muwazi.

Amesema tu kwamba, namaliza kwa kunukuu Msahafu, Ayubu 19-25: "Lakini mimi najua ya kuwa mtetezi wangu yu hai na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi, atanishindia".

Hii ndiyo barua niliyoandikiwa mimi ambayo ni mbaya zaidi kuliko hata hiyo iliyoandikwa na *TRA*. Kuniambia kunipeleka kwa Ayubu. Mimi nafanya kazi hapa kwa mujibu wa Sheria,Taratibu na Kanuni kama nilivyoapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Ayubu bila Ayubu tutaonana mbele ya safari. Lakini hapa niliapa kutetea Sheria, Kanuni, Taratibu na mimi kama Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, nimeridhika kabisa *beyond any doubt* kwamba, Shirika langu limefanya vizuri na liendelee kufanya hivyo kwa wengine waliobaki na watakaokuja nyuma na kwamba huu ndiyo msimamo wenu Waheshimiwa Wabunge. Lakini huyu mama aendelee kuomba kwa Ayubu na mimi nitaomba Mungu vilevile ili tusiendelee kusononeka kwa sababu

hakuna mtu aliye na nia mbaya wala husuda wala ukabila wala uovyo ovyo tu kufanya kazi bila kutafakari. Namwomba Mheshimiwa Mbunge, asizungumze habari za peleka Kamati kule kwa sababu kwa kweli makabrasha ni mengi na hili somo tulimalize tuendelee kusali tu kama ni kuomba kwenye Biblia au wapi, tugange ya mbele.

Nilisema niliseme hili kwa sababu kitu kilichotoka hapa ni kama kuna mtu aliyeonewa kifo au kwa kweli mimi sikuridhika hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa *Finance Bill,* kama nilivyousoma na kutetea mbele yenu sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Kicheko)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyopo kama alivyosahihisha mwenyewe, anaomba Muswada mkubali usomwe mara ya pili. Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2004** ***(The Finance Bill, 2004)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza, Muswada huu una vifungu vile vidogo vidogo jumla ya 62. Kwa hiyo, tukisema tuhoji kifungu kwa kifungu ni mara 62. Sasa tutafanya vile ambavyo mara nyingi tunafanya. Tutahoji kwa sehemu na kila mtu ana uhuru wa kuweza kuhoji wakati wote ambao tutasema kisehemu. Katibu endelea.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39
Kifungu cha 40

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa tano wa haya marekebisho, liliulizwa hapa swali na Mheshimiwa Job Ndugai, juu ya ile *Schedule, which is which,* kwa sababu maneno yameandikwa sawasawa kule juu. *Tax Payable where incomplete records are kept, Schedule* la katikati na *schedule* ya mwisho kule kulia, *Tax Payable where in complete records are kept.* Mheshimiwa Mbunge, akauliza *which is which* na kweli nafanya marekebisho pale kuna kosa la uandishi. Ile ya mwisho ya kulia ndiyo ilipaswa kuandikwa *Tax Payable where complete records are kept* na hiyo hiyo inabaki *incomplete* na hiyo ya katikati *incomplete* ya kulia ni *complete records.* Naomba kuwasilisha.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakiri aliyosema Waziri wa Fedha kwamba, tumefanya kazi kwa muda mrefu vizuri sana na hatuna matatizo na ndiyo maana nilikuwa nasitasita kuzungumza wakati wa hotuba yake ya kwanza. Sasa kilichonistusha mimi ni ile barua kwa sababu nilichangia tarehe 29 tarehe 2 ikaandikwa barua na ukichukua na yale majibu aliyoyajibu Waziri wa Kazi,

nikapewa nakala. Kwanza, mimi sikuwepo kwenye kesi, angepewa nakala aliyehukumu, Waziri wa Kazi kwamba, hatukuikubali. Lakini maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, yameniridhisha. Mimi sikujua yalivyokuwa huko ndani. Kwa hiyo, mimi namwomba Waziri wa Fedha, tuendelee kama kawaida. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, amekubali ameridhika na mahusiano yenu yaendelee vizuri.

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 55
Kifungu cha 56

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2004**
***(The Finance Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Stephen Kahumbi, vya hapa Bungeni ni vya Bungeni, ameonyesha ukomavu wake wa kisiasa na kama mtu mzima, kwa hiyo, yanabaki hapa hapa, huko nje tunatafuta soda tunakunywa hasa kesho usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2004 *(The Finance Bill, 2004),* kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shughuli za leo tumemaliza. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.17 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa tarehe 6 Agosti, 2004 saa tatu asubuhi)*